MASWALI NA MAJIBU

Sijui wapi. Wao—wao labda huenda hawakuiandika. Walisema, "Isaya 4:24." Sas a, Isaya 4 ina vifungu sita pekee, kwa hivyo mini . . . sijui kama ulimaanisha Isaya 5:24. Lasema, "Nini maana ya Andiko hili, na litatimia lini, Isaya 4:24?" Na Isaya 4 ina vifungu sita. Kama waweza . . . Ye yote yule aliyekiandika, ukiwaza sasa, labda, na uliandike tena, nawezi kulifikia, mwaona. Sijui ulikuwa unataja wapi, Isaya 4:24, nini maana ya Andiko hili na litatimia lini?"

2 Sasa, sitawakawisha sana. Nina . . . Vema, asante, ndugu. Na nina—ninaenda mahali fulani, na hili . . . Mwajua, nilikuwa nikiwaza, nilikuwa na andiko hapa . . . kunradhi, barua toka kwa Bw. Baxter. Na kabla hatujaanza ibada asubuhi hii, kushughulikia haya, ni—ningependa ninyi ku—kuomba pamoja nami kwa muda mchache.

3 Ni—nilikuja ibadani na nia njema sana kuenda katika—ibada yangu ngambo, katika siku chache tu zijazo. Sasa napata barua toka kwa Ndugu Baxter, Ndugu Cox alinisomea kwenye simu usiku uliopita na kunipa asubuhi, kuwa wanajaribu kuiahirisha tena sasa tena. Nami—nami sijui kama ni Shetani anayejaribu kunizuia au ni Mungu anayengoja wakati ufaao. Si—sijui. Wanataka kuiahirisha kidogo, na wamekuwa wakiiahirisha tangu Oktoba. Oktoba, Novemba, Januari, hii ni karibu miezi minne sasa ambayo wamekuwa wakiiahirisha.

4 Na sasa ono limekuja, imeandikwa hapa katika Biblia yangu yale hasa yatakayotendeka; lakini sijui lini. Sasa, nimewaambia watu tu (kwa nia njema) yale waliyoniambia, kwamba wawe tayari wakati huu sasa.

5 Sasa watu hudhani kuwa, najua, kuwa mimi si mwaminifu kuhusu hiyo, "Ee, nini . . . ataenda lini . . . Yeye ataenda lini?"

6 Lakini nipatapo barua hizi nao wananiambia, "Vema, hauwezi kufanya hivyo hata sasa, sharti *hili* lifanywe, na yapasa *hili* litimizwe." Ndipo si— . . . na—nasikia vibaya kusimama mbele za watu. Sijui la kufanya. Lakini jambo moja, nitafanya hili, nanyi nyote pamoja nami; nitalikabidhi kwa Mungu, na kusema, "Sasa, Bwana, ukiwa tayari, mimi hapa," Ona? Na niki . . .

7 Wakati mwingine ni kanisa lisilo tayari, sasa ni hati za kusafiria au kitu kinginecho. Mwajua kuna vitu kama hivyo. Labda ni Shetani anayejaribu kufanya hilo. Kwa hivyo tunapoomba asubuhi hii . . . Na kila wakati unapokuwa ukiomba juma hili lote, u—uniombee na kumwomba Mungu a . . . Kama ni Shetani, amwondolee mbali. Ona? Na kama ni—ni mapenzi Yake, anizuia hapa. Ona? Yeye yuajua la kufanya hasa. Huenda

kukawa na kitu fulani anachotenda hapa, kurekebisha mambo. Sitaki kamwe kuenda mbele Yake. Ee! Unapofanya hilo, ni la kuogofya. Ona? Kwa hivyo—najisikia tu hilo ni . . . hilo—hilo huenda likawa . . . Sijui niseme nini, kwa sababu sijui.

8 Kama tu vile ndugu yetu mpendwa, George Wright. Wengi wenu mwajua hali zake, sivyo? Nanyi mwajua madaktari wamemkatia tamaa, naye ilidhaniwa angekufa juma lililopita, au hapo kabla, ona, Ndugu George Wright. Nilienda chini kule kumwona, na nilipokuwa chini kule niliomba na kuomba kwa unyofu kadiri nilivyoweza kumwombea. Na ndipo nikaja nyumbani na kushangaa ingekuwaje. Na baada ya siku chache, vema, ni—nilipata ono Jumatatu iliyopita asubuhi, nami nangoja . . .

9 Sasa, kuna—kuna mwanamke niliyemwombea aliyekuwa na kansa, nami nilimwona akisimama naye—naye ange . . . Walimpasua, alikuwa kansa tu—tupu, wakamshona tu. Ona? Bali yeye ataishi. Najua hilo.

10 Lakini sasa, Ndugu George Wright, sikupata hilo ono dhahiri. Nilikuwa ninakuja . . . Ono lile lile, nilipokuwa nikija niliona kwa—kwake, nyumba yake. Na upande wa kushoto wa nyumba kuliko na miti, mti wa majini, papo hapo juu niliona tita la taka, karibu kubwa kama ngumi yangu, likifingirika. Nami nikasikia yule Malaika aliyekuwa amesimama kando yangu, akisema kitu fulani kuhusu kaburi na Ndugu George.

11 Sasa, ilikuwa au hili, kuwa ilikuwa kaburi la Ndugu George walilokuwa wakichimba, au yaonekana kwangu . . . Sasa, kumbuka basi, singeeleza hili . . . na kwa kuwa naamini tuna maikrofoni zinazofanya kazi humu, au vinasa sauti, samahani. Lakini sasa nataka kulieleza dhahiri, ningependa, kama nilivyofanya kwao, nafikiri ilikuwa hii . . .

12 Kulikuwa na kundi la watu chini pale waliokuwa wakimcheka kwamba yeye aliamini kuwa Mungu atamponya baada ya daktati kusema . . . pata nafuu. Vema, hawezi, ona, damu iliyovilia imeingia katika mapafu yake, na anatema damu, na kadhalika. Yeye alisema, "Punje ndogo tu ya kwanza itakapoingia moyoni mwake au kichwani mwake, itampoozesha au itamuua." Ona? Na yeye ana umri wa miaka sabini na miwili, amepitisha wakati aliokusudiwa.

13 Lakini naamini ilikuwa hivi, kwamba yeye atachimba kaburi la baadhi ya wale waliokuwa wakimcheka, achimbe kaburi. Na sasa, sikujua kuwa yeye alikuwa mchimba makaburi, lakini ndivyo alivyo. Mimi . . . Na mwaona? Nami nilidhani kuwa yeye alichimba makaburi yao, hiyo ndiyo kazi yake. Na ilionekana kama kulikuwa na kitu fulani kuhusu kaburi na kuchimba kaburi, au—au kitu kama hicho, na Ndugu George Wright.

14 Nami nalimsihi Bwana sasa, kwa karibu usiku munne, kunionyesha tena akipenda. Likaja yapata saa moja au saa

mbili asubihi moja. Kwa hivyo natumai Yeye atalifanya dhahiri. Lakini naamini kwa moyo wangu wote . . . Sasa, hii ni kwamba nilikuwa sahihi niliposema kuwa yeye atawachimbia kaburi baadhi yao, wale wanaomcheka, kama nililipata dhahiri. Lakini sina hakika sana. Lilikuwa jambo fulani kuhusu kuchimba kaburi, na Ndugu George Wright. Nadhani yeye alikuwa achimbe kaburi la mtu fulani aliyekuwa akimcheka.

15 Sasa, Mungu ni upendo, na, ee, tunampenda kwa mioyo yetu yote.

16 Sasa, asubuhi hii hatutaki kuchukua wakati wetu mwingi hapa kwa maswali haya. Nitayajibu vema kadiri nijuavyo. Sasa, marafiki, naweza kufanya makosa mengi sana kwa mambo haya. Mimi tu—mimi ni mwanadamu tu kama wengine wetu wote. Na Ndugu Neville, au ye yote wa hawa wahudumu wengine, na kadhalika, wanaweza kuyajibu kama niwezavyo mimi. Lakini, nafanya hili kwa kusudi fulani, kujaribu kupata kile kilicho mioyoni mwa watu.

17 Ndipo kama nikiona watu wanne au watano wakivutania jambo moja ndipo nadhani, "Ahaa! Haya basi. Ona, najua ilivyo sasa, maswali madogo-madogo kadha kanisani." Na sasa hebu tusahau hayo—hayo maswali madogo. Na jambo kuu zaidi ya yote ni kuweka kanisa katika amani na upendo wa Mungu, na kusonga mbele, tukiweza sote kuamini kuwa Damu ya Yesu Kristo hutuosha na dhambi zote na maovu yote. Kama mwanamke anayeketi kando yako, au mwanamume anayeketi kando yako, kama yeye haamini kwamba Yesu hakika ata—atarudi tena akionekana, hebu tuliamini na kusonga mbele, haidhuru. Sisi hatukubaliani nao kwa Maandiko. Lakini hebu tufanye kanisa liendelee kwa amani, kwa sababu ndani mle tutapata watu wengine zaidi. Lakini kanisa lisipokuwa na amani, ndipo una—unadhuru kanisa, ndipo unadhuru wajibu wake. Ninyi . . . ni . . . hauwezi kufanya hivyo. Lakini tuwezapo kukubaliana kwa jambo moja, kwamba Damu ya Yesu Kristo yatusafisha dhambi zote (naam) na dhambi inapoondolewa, ndipo sisi—sisi tu karibu sana nyumbani, tumekaribia, Ndugu Neville. Damu i . . . tunapobarikiwa.

18 Nina ndugu; ndugu yangu halisi. Lakini, lo, jinsi hatukubaliani; enhe, vibaya sana. Lakini, si hoja, sisi ni ndugu.

19 Sasa, nilikuwa nawaza juma hili, juma lijalo, kama sitaenda ng'ambo, labda . . . Ndugu Cobbles aje, naye alitaka kuanzisha mikutano katika Louisville, naye alitaka apate pale Armory ambapo tulikuwa na mkutano wetu mdogo wa uponyaji pale usiku mmoja. Na Bwana alitenda mambo ya ajabu. Na kwa hivyo . . . Lakini ndipo nikasikia kuwa wale Ndugu toka Del Rio, Texas, ndugu wa Jessup, wana ibaada katika Louisville nao wana wanenaji wao bora sana kule kwa majuma yajayo. Na kasema yeye hakujua angeondoka lini. Charles, naamini,

ndiye atakayekuwa kule juma lijalo, nami hakika singeanzisha mkutano wa ufufuo po pote hali mkutano wa aina hiyo unaendelea.

20 Nao pia wana mikutano ya uponyaji. Na kwa hivyo mkutano wa uponyaji ni jioni, jioni hii. Na kwa hivyo singependa kuanzisha mkutano na—na wao wanao mkutano pale, sababu najua inamaanisha nini kuwa mahali fulani na ni . . . Ee, mwajua, ningalikuwa na mkutano na mtu fulani aruke juu na kuanzisha mkutano mdogo hivyo. Halionekani zuri, hiyo si tabia nzuri, mwajua. Kwa hivyo tutangoja tu hata baadaye, labda Bwana atatusaidia. Yeye atatusaidia, haidhuru, na kwa hivyo tunaamini na kuvumilia na kuwa waaminifu kwa Mungu.

Basi na tuombe:

21 Baba, uliye Mbinguni, hebu na baraka Zako zing'ae juu yetu sasa ninapoenda kujibu maswali haya. Ewe Mungu, tu . . . kunayo baadhi yayo hapa ambayo sijayatazama bado, na mawili au matatu ambayo nili—nilisoma muda mchache uliopita. Naomba, Baba, kuwa utanisaidia na unipe hekima na ufahamu nipate kunena tu yaliyo sahihi. Tujalie, Baba. Nami na niwe na Hekima Yako na Roho Mtakatifu ashuke sasa na atoe hekima inayohitajika. Tubariki sote pamoja leo, Bwana, kama kundi hili ndogo la maskani hapa.

22 Mbariki ndugu yetu mpendwa, Ndugu Neville, hapa Baba, yeye anafanya kazi, mchungaji humu katika uwa nja wa mchungaji, a—ambaye anajaribu kuongoza kondoo kwenye majani mabichi na malisho mazuri, au nje majini na kuwarudisha katika mti wenye kivuli, na kuwashughulikia wagonjwa na wenye mahitaji na waliolemaa na wale walio wachovu na kujaribu kuwatibu na kuwaleta, wapate kuwa kondoo halisi. Ewe Baba, naomba kuwa utambariki. Mpe hekima na maarifa na ufahamu.

23 Na tusaidie sisi sote pamoja sasa, Baba, ndipo tutakutukuza. Katika Jina la Yesu. Amina.

24 Sasa, katika baadhi ya haya hapa, nitayafikia mara tu baada ya kitu fulani . . . sehemu mbalimbali za Maandiko ambazo—zinazoyapasa. Na sasa tunaanza tu kwa machache, na kujibu moja kwa moja hata tuweze kupata—kufikia mengi tuwezavyo. Nami naamini tunaweza kuyafikia yote, nami nitatazama hapa ili tutoke mapema.

25 Jambo la kwanza ni swali tu, swali wazi kabisa.

8. Nilibatizwa nilipokuwa na umri wa miaka kumi na mitatu. Je, yanipasa kubatizwa tena?

26 Naam, hilo—hilo ni swali ndogo nzuri kuuliza. Vema, sasa, rafiki, kila mara huachia hilo mtu binafsi.

27 Kumbuka, sijui . . . Kunalo moja ninalojua yule aliyeliandika, hilo ni hili papa hapa, na mtu huyo mwenyewe

ndiye aliyenipa. Na mtu fulani aliniuliza swali fulani kule nyuma ambalo yanipasa nijibu, hawakuliandika, nami nilisema, "Kama nina wakati wa kutosha baada ya haya hapa nitalijibu."

28 Lakini sasa hili hapa, "Niba . . . Nili . . . "

Nilibatizwa nilipokuwa na umri wa miaka kumi na mitatu. Je, nibatizwe tena?

29 Kama umekuwa Mkristo wakati huu wote, tangu ulipokuwa na umri wa miaka kumi na mitatu, anayemwamini Kristo, ningekaa tu kama ulivyo. Singefanya hivyo sasa, kama Mungu amekubariki na kukupa Roho Mtakatifu tangu wakati huo.

30 Na ubatizo ni—ni—ni mfano tu, ni ku—kuonyesha ulimwengu (au kusanyiko uli—ulio nao wakati huo) kuwa wewe, mbele ya mashahidi, unathibitisha kwamba umekwisha amini kuwa Mungu alimtuma Mwanawe naye akafa na kufufuka tena siku ya tatu, na ulizikwa ndani Yake na umefufuka kuenenda katika upya wa uzima. Na watu wale waliokutazama ulipobatizwa watakutana nawe Hukumuni. Ona.

31 Ndiposa baadaye, kama mtu fulani (mgeni) akisema, "Ulibatizwa?"

32 "Naam nimebatizwa na . . . katika mauti na kuzikwa kwa Bwana wetu."

33 Ona, nadhani ubatizo . . . Ee, nasema ni muhimu, singetaka kusema si muhimu. Lakini ni muhimu kwa sababu ni . . . kila Amri ya Mungu ni muhimu. Je, sivyo? Ni muhimu kwamba hatuna budi kubatizwa. Yesu alitupa matamshi haya katika Mathayo Mt. au Marko Mt. 16, Yeye alisema, "Enendeni ulimwenguni kote mkaihubiri Injili, aaminiye na kubatizwa ataokoka." Na alipokuwa akiongea na Nikodemo, Yeye alisema, "Mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho hataingia katika huo Ufalme." Huna budi kubatizwa. Naamini katika kuzikwa katika maji mengi, kwa ubatizo, katika Jina la Bwana Yesu Kristo, na kufufuka tena katika upya wa uzima, kuzitii Amri za Mungu.

34 Lakini, unasema, "Ndugu Bill, je, umewahi kumbatiza tena ye yote, aliyebatizwa alipokuwa mtoto mchanga na ndipo akabatizwa tena?" Mara nyingi.

35 Kwa hivyo mna—mna Andiko katika Ufunuo, sura ya 2, akinena kuhusu kanisa, Yeye alisema, "Ukatubu na ukafanye matendo yako ya kwanza tena." Na wengi wao hutafsiri Andiko hilo kusema hivi, kwamba hiyo yamaanisha ati urudi nyuma tena na kurudia jambo lile tena. Vema, kama utatambua rafiki Mkristo mpendwa . . .

36 Sasa, sikatai kukubaliana na hili sasa, ona, kwa sababu pa kubatizia pamejaa maji. Tuko tayari kumbatiza ye yote anayetaka kubatizwa wakati wo wote. Lakini hatukatai kukubaliana. Kwa hivyo ukitaka kubatizwa, kama hicho ndicho kitu kinachokuzuia na unajisikia kama inakupasa, nenda

ukafanya vile. Naam. Enda ukafanye hivyo. Usiache lo lote likuzuie, jiridhishe kabisa.

37 Kama tu u—ulichukua kitu fulani miaka mingi iliyopita, na unaona kwamba inakupasa kurekebisha hilo, nenda ulirekebishe. Haijalishi ni nini. Nyosha kila kitu. Kwa sababu utafikia kitu kile, na hutaendelea mbele zaidi hata utakapokiondolea mbali, waona. Yatupasa tu kuweka kando kila mzigo mzito, na dhambi ile ituzingayo kwa upesi.

38 Na ukitaka kubatizwa tena, endelea, ndivyo ipasavyo kufanya. Nimebatiza wengi tena.

39 Lakini sasa kwa hilo Andiko unalolitaja, hilo halikuwa likimwambia mtu binafsi, kanisa. Ona, kanisa, yale waliyokuwa nayo mwanzoni. Nao walisema, "Usipotubu na kufanya matendo ya kwanza tena," anzia kule nyuma tena na upate kitu kile. Yeye analiambia kanisa, "Usipotubu na kurudi nyuma tena," vema, basi, Yeye angeondoa kile kinara.

40 Na ukitaka ubatizwe, na kama ulikuwa umebatizwa ulipokuwa na umri wa miaka kumi na mitatu, au umri wo wote, basi, ba—batizwa kama linakukwaza.

41 Lakini sasa kusema hilo Kimaandiko ningesema kuwa yakubidi ubatizwe tena, kuna njia moja pekee ya Kimaandiko ambayo ninge—ningetangaza kuwa watu walibatizwa tena. Kuna Andiko moja pekee katika Biblia nzima ambapo watu walibatizwa tena, napo ni wale waliobatizwa na Yohana Mbatizaji kabla Roho Mtakatifu hajakuja. Paulo, katika Matendo 19:5, aliwaambia hao kwamba iliwabidi wabatizwe tena kwa Jina la Yesu Kristo, ili wampokee Roho Mtakatifu. Ona?

42 Sasa, sasa, si lazima kubatizwa ili upokee Roho Mtakatifu, kwa sababu unaweza kumpokea Roho Mtakatifu moyo wako ukiwa sahihi. Ona? Kwa sababu, kwenye Matendo 2, Petro alitoa utaratibu wa—utaratibu wa "Tubuni mkabatizwe katika Jina Lake Yesu Kristo, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu." Lakini basi, katika Matendo 10:49, Mungu aligeuka na kuwapea Mataifa ubatizo wa Roho Mtakatifu kabla wao hawajabatizwa kamwe. Mwaona? Kwa hivyo, mwaona, ni hali ya moyo wako.

43 Ndipo Petro alisema, "Ni nani awezaye kukataza maji hawa wasibatizwe, watu waliopokea Roho Mtakatifu vile vile kama sisi hapo mwanzo?" Mnaona? Kwa hivyo basi a—akawashurutisha kubatizwa kwa Jina la Yesu Kristo.

44 Ndipo Paulo, katika Matendo 19, alisema . . . Paulo akisha kupitia nchi za juu ya Efeso, akakutana na wanafunzi fulani, naye akawaambia, "Je! mmepokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini?"

45 Wao wakasema, "Hata kusikia kwamba . . . hatukujua kwamba kuna Roho Mtakatifu."

Akasema, "Basi mlibatizwa kwa ubatizo gani?"

Walikuwa wamebatizwa. Walisema, "Tumebatizwa kwa ubatizo wa Yohana."

46 Yeye alisema, "Yohana alibatiza kwa ubatizo wa toba, akiwaambia kwamba, 'Yawapasa kumwamini Yeye atakayekuja,' ambaye ni Bwana Yesu Kristo." Nao waliposikia hayo, wote wakabatizwa tena kwa Jina la Yesu Kristo. Ona? Kwa hivyo basi hilo ni . . .

47 Sasa, kuhusu hili, ni . . . Lakini kusema tu ulibatizwa kwa ubatizo wa Kikristo ukiwa na umri wa miaka kumi na mitatu, na umeishi maisha ya Kikristo kote, au kama umeanguka mara chache . . .

48 Sijui kama wana . . . Kwa kuanguka, sijui, natumai mtu fulani angeuliza—kuniuliza mimi hilo. Lakini kwa kuanguka, kumbuka, unaanguka kila siku. Hauwezi kujizuia kamwe. Vema, "Unapoanguka," ni kwa watu walio kanisani, bali si mbele za Mungu. Ona? Unaanguka kwa Kristo, bali si kwa Mungu. Kwa sababu ungalitenda dhambi kweli, umepotea. Lakini wewe huanguka kila mara. Ilimbidi Paulo afe kila siku. Sivyo? Ilimbidi kufa kila siku na kutubu kila siku, kutubu daima. Ona? Na kama ilimbidi Paulo kutenda hilo, ndipo yanibidi nami pia. Nawe je? Naam. Kwa hivyo . . .

49 Lakini sasa, kama—kama ume—umekombolewa na unajisikia kuwa Da—Damu ya Yesu Kristo inakuosha dhambi, basi ni—ni . . . na umeishi maisha ya Kikristo, si—singedhani inafaa. Lakini ukitaka kubatizwa, basi, vema, tutafurahi kufanya hivyo.

50 Sasa hapa kuna kijikaratasi kidogo ambacho mtu fulani alinipa nyuma kule:

9. Kanisa litakuwaje Injili iwarudiapo Wayahudi?

51 Sasa, mtu aliyeandika hili, alikuwa akitaja Luka hapa, ile . . . Yeye—yeye aliniambia, ndugu yangu, kuwa alikuwa akitaja ambapo ilisema, "Ma—mataifa watakanyaga kuta za Yerusalemu hata majira ya Mataifa yatakapotimia." Hiyo ni Luka 21:24. Sasa sikiza kwa makini na hili huenda likalipata. Swali nzuri! Ajabu!

> *Lakini hapo mtakapoona Yerusalemu umezungukwa na majeshi, ndipo jueni ya kwamba uharibifu wake umekaribia.*

52 Sasa, hebu tulishike hili kwa makini sasa. "Ule uharibifu umekaribia mtakapoona mji wa Yerusalemu umezungukwa na majeshi." Sasa, hilo hapo limetatiza sana, huku watu katika . . . Lakini liendee kwa mawazo ya kihistoria na Biblia.

53 Sasa, ndugu Wa-Adventist, ndugu wa Seventh-day Adventist, wanaamini kuwa—kuwa Yerusalemu tena

utazungukwa na majeshi. Vema, sasa, hilo huenda likawa kweli, kwa sababu mara nyingi Maandiko yana maana zaidi ya moja.

54 Na wangapi wanajua Maandiko yana maana zaidi ya moja kwa kila unabii? Hakika! Naam, bwana. Yatanena na kulikusudia kwa wakati *huu* hasa, na kugeuka na kujirudia tena na tena *hapa* mahali fulani. Ona? Kama... Nami nitataja moja ya hiyo kama naweza kukumbuka upesi. Ee, naam, hapa kuna moja katika Luka... katika Mathayo 2, ilisema, "Na Yesu akaitwa toka Misri iii yatimie yale yaliyonenwa na nabii akisema, 'Na... nalimwita mwanangu... toka Misri.'"

55 Sasa, unabii huo unaotajwa nyuma mle na nabii ulikuwa hasa ukitaja *Israeli* (ambaye alikuwa mwana wa Mungu). Yeye aliitwa kutoka Misri. Naam, katika—katika Mwanzo na Kutoka. Lakini uli—ulikuwa ukitaja hayo pa—pale, lakini ulikuwa utajirudia tena. "Toka..." Israeli alikuwa mwana wa Mungu. Mwajua hilo. Yeye alimwambia Farao, kasema, "Wewe..." kasema kuwa "Wewe—wewe..." alichomfanyia mwanawe, kuwa Yeye angechukua uhai... Yeye hangemkubalia Mwanawe aende, kwa hivyo Farao... Mungu alimchukua mwana wa Farao toka... na... au malaika wa mauti usiku huo. Kwa hivyo ina maana zaidi ya moja.

56 Na kwa hivyo, sasa, Yerusalemu, ilipozungukwa na majeshi, bali, bila shaka, kihistoria, hiyo ilikuwa karibu 96 B.K. wakati Tito alipouzingira Yerusalemu. Lakini sasa tazama haya kwa makini, waweza kuona tofauti yake, naamini kuwa Yerusalemu utazingirwa na majeshi tena wakati wa mwisho. Lakini naamini hili hapa lilikuwa likilinganisha na... wakati ule Tito alipowazingira hao, uharibifu ulipotokea.

57 Sasa, "uharibifu," kunena... ilikuwa wakati Danieli, yule nabii... "limesimama katika Patakatifu." Tazama, yeye alisema, "mtakapoliona chukizo la uharibifu, limesimama katika patakatifu." Ona, "chukizo," *chukizo* ni "uchafu." "La uharibifu," *uharibifu* ni "kuondolea mbali," ni "kuangamiza." "Mtakapoonapo chukizo la uharibifu limesimama katika Patakatifu," lilitimia kimaandiko wakati Tito aliupozingira mji wa Yerusalemu, akatwaa...

58 Mwanzoni mwa sura hii ambapo walimuuliza Yeye, "Wakati wa mwisho utakuwa lini? Nayo ni nini dalili ya kuja... kwa Kristo?" Nao wakamwambia kuhusu hekalu, jinsi ilivyokuwa, ilivyopambwa vizuri kwa mawe makuu na kadhalika.

59 Yeye akasema, "Kutakuja wakati ambapo halitasalia jiwe juu ya jiwe, ambapo hili litabomolewa." Yeye alianza kuwapa ishara na maajabu. Ndipo, Yesu akinena sasa, arudia sasa Danieli, kutimiliza, kwa sababu unabii wote hauna budi kushikamana na mwingine. Maandiko yote hayajatanguka po pote.

60 Yesu alisema, "Maandiko hayawezi kutanguka." Amina. Na pale. . .Je, naenda Mbinguni? Hakika, ninaenda! Maandiko hayawezi kutanguka. Kwenu msioamini ishara na miujiza na maajabu, mtaliepukaje Andiko hilo? Maandiko hayawezi kutanguliwa zaidi tu ya Kristo awezavyo (juu hapa), awezavyo kuondolewa. Kama tu mwili Wake mkuu kule juu, na kila mwenendo wa mwili Wake huonyesha mwenendo fulani chini hapa duniani, haina budi kuwa vile. Ndipo kama Kristo. . .kama. . .Uponyaji wa kiungu, nguvu za Mungu zinapoondoleewa kwa kanisa linaloonekana, au kanisa la kiroho hapa duniani, ndipo zimeondolewa kwa Kristo. Hawezi tena. . .

61 Lakini, ee, mfano jinsi gani wa Mzabibu wa kweli, nasi tu matawi katika Mzabibu huo. Ona? kama tu vile Mzabibu uenendavyo, vivyo hivyo matawi pia. Sivyo? Ni nzuri vipi basi kwa mwili Wake mkuu, ee, ile mikono Yake mikuu inayotokwa na damu na machozi yanayodondoka, na ubavu Wake unaotokwa na damu, na mgongo Wake uliopigwa mijeledi umeangikwa juu ya dunia *hivi* kati ya Mungu (Baba) na viumbe wa dunia hii, aki—akiwasihi na kuwapenda wao wakati tu mwili Wake unapoanza kusonga mbele na kupata mamlaka, yamekirimiwa Kanisa.

62 Kama tu vile Yeye angalisema, "Nitasogeza mikono yangu upa—upande huu," na mwili Wake wa kuonekana unasonga. "Enda hapa ukahubiri Injili," utaona Kanisa hilo likienenda moja kwa moja. Kwa sababu, kivuli changu chapaswa kusonga pamoja na mkono wangu. Amina. Sivyo? Amina. Ee, lo, ninapowaza hilo! Ni Yeye yule, mwili Wake ukisonga mbele, "Enendeni duniani kote mkadhihirishe Mamlaka hayo." Haijalishi kama tunaacha theologia yetu na mafundisho na mengineyo kama hayo, tunaanguka vibaya mno. Lakini sasa mkono wa Mungu u—unaenenda, ishara na maajabu yanatendeka. Naam, jamani!

63 Yesu alisema, chini kule alipokuwa akitoa pepo. . .Bila kuenda nje ya swali hili, sasa, kwa muda mchache tu. Lakini Yesu alisema, alipokuwa akitoa pepo, alisema, "Na wana wenu wanatoa pepo kwa uweza gani?" Basi, kama Mimi nikitoa pepo kwa kidole cha Mungu, wana wenu je! huwatoa kwa nini? Kama mna msuada bora tuonyesheni sisi." Ona? "Kama Mimi nikitoa pepo kwa kidole cha Mungu. . ." Amina. Fikiria tu, "Kidole," cha Mungu. Hiyo ni Mungu juu ya Kristo; Kristo juu ya kanisa. Ndiye huyo Mungu, Baba, asema jambo *fulani;* ndipo Mungu, Mwana, anausogeza mkono Wake na kivuli kinaufuata. "Kama Mimi natoa pepo kwa kidole cha Mungu, wana wenu je! huwatoa kwa Nini?"

64 Tazama, nawatakeni ninyi kutambua. Ee, haijalishi ugonjwa ni mkubwa vipi au majuto ni mengi namna gani Pepo awezayo kuweka juu yako, inahitaji kidole Chake kuviondoa. Ee, jamani! Tazama hayo mabega makubwa yenye nguvu na mikono na

misuli. Kidole chake tu kitaondoa kila ugonjwa na kutoa pepo. Na Pepo ni kitu kidogo vipi! Yeye achukua tu kidole Chake na kumwondolea mbali. "Kama mimi kwa kidole cha Mungu . . . "

65 Sasa hebu niwaonyesheni baadhi ya upendo wa Mungu. Lakini kondoo alipopotea, Yeye hakutumia kidole Chake, alimweka mabegani, na akatumia mwili Wake wote, mikono, kondoo begani Mwake. Sehemu ya mwanadamu iliyo thabiti sana, na yenye nguvu ni mabegani mwake na mgongoni. Mwajua hilo. Kwa maana misuli yake yote ya mkono na misuli mingineyo inaanzia pale, na Yeye humtwaa kondoo wote; na kumweka juu begani Mwake na hapa Yeye yuaja, si kwa kidole Chake, kumwondoa maskini, shetani wa kale, lakini hapa Yeye yuaja na aliye Wake . . . misuli Yake yote ya miguu Yake, misuli Yake yote ya mikono, akienenda jangwani kote, akimbeba yule kondoo aliyepotea kwenye bega yake. Jamani! "Kama mimi natoa pepo kwa kidole cha Mungu, watoto wenu je! huwatoa kwa nini?" Ee, haleluya! Jamani!

66 Vema, turudie somo tena:

> *Lakini hapo mta . . . kapoona mji wa Yerusalemu umezungukwa na majeshi, . . .*
>
> *Ndipo walio katika Uyahudi na wakimbilie milimani, na walio katikati yake wasikimbie nje, na . . . walio katika mashamba wa . . . ingie.*
>
> *Kwa kuwa siku hizo ndizo za mapatili—mapatilizo, yatimizwe yote yaliyoandikwa.*
>
> *Ole wao wenye mimba na wanaonyonyesha, katika siku hizo! kwa kuwa kutakuwa na shida nyingi katika nchi, na hasira juu ya taifa hili.*
>
> *Wataanguka kwa ukali wa upanga, nao watatekwa nyara na kuchukuliwa katika mataifa yote . . .*

67 Tazama jinsi Maandiko yalivyo mazuri hapa kulifanya dhahiri. Kwanza, "Kwa makali ya panga." Mara ya pili itakuwa kwa bomu la atomiki. Ona? Lakini hii ni kwa ukali wa upanga, na Wayahudi wangechukuliwa mateka kwa mataifa yote. Haitakuwa hivyo tena, watakusanyika katika Palestina wakati wa mwisho. Ona? Hili lilikuwa likitaja siku zilizopita. Na lilo hilo hasa lalingana na historia, ilitimia tu vivyo hivyo.

68 Walichukuliwa kwa mataifa yote. Kila taifa chini ya Mbingu siku hizi, utawapata Wayahudi. Ee, kila taifa! Uende Uchina, na utakuta Wayahudi. Uende Urusi, utakuta Wayahudi. Uenda kwenye visiwa vidogo-vidogo, utawakuta Wayahudi. Wametawanyika katika kila taifa! Ni nini? Unabii wa Mungu. Mungu alikusudia hayo. Na Wayahudi hawa ni jiwe la kuonyesha mwendo wa njia, ndugu. Unapowaona . . .

69 Najua wamepofushwa na kuongozwa vibaya, na kudanganywa na kadhalika, lakini walidanganywa na Mungu

ili wewe na mimi tupate kuona. Naam. Lakini nitasema hili kwa roho ya unabii, kwa Biblia, kwamba, majira ya Wayahudi kurudi nyumbani yamekaribia. Naam, bwana. Yeye aliufanya moyo wa Hitler uwe mgumu, akawafukuza Ujerumani; akaufanya mgumu moyo wa Mussolini, akawafukuza toka Urusi. Yeye anawafukuza kila mahali, kama alivyofanya katika siku ambazo aliwatoa. Na ndipo walipofika jangwani pale na walikuwa tayari kuvuka, nini kilitendeka? Mungu alizuru nchi kwa mapigo makuu na kadhalika. Ambayo Yeye atarudia tena akitumia wale watumishi Wake wawili, ile mizeituni miwili ya Ezekieli na pia ya Ufunuo 11. Yeye atarudia ishara hizo na maajabu.

70 Watazame hao mashahidi wawili katika Ufunuo 11, "Nitawapa uweza hao mashahidi Wangu, nao wataifunga mbingu katika siku za unabii wao. Watatuma mapigo juu ya nchi wapendavyo." Ndio hao, wale mashahidi wawili katika siku za mwisho.

71 Najua mafundisho ya kisasa ni kwamba, "Hiyo ni Agano la Kale na Agano Jipya." Hilo ni kosa! Hilo ni kosa!

72 Ndio hawa wale mashahidi wawili, hiyo bila shaka ni kurudi kwa Musa na Eliya. Na unatambua nyuma kule, hapana mmoja wao...Musa, alikufa, lakini alienda wapi? Ilimbidi afufuke tena. Naye Eliya aligeuzwa hata bila kufa. Itambidi afe, kwa sababu kila kiumbe hakina budi kufa, kwa hivyo hana budi kurudi tena. Basi hao ndio wale mashahidi wawili.

73 Sasa tazama:

> Watakanyaga...*Wataanguka kwa ukali wa upanga,*...(kifungu cha 24)...*wa upanga, nao watatekwa nyara na kuchukuliwa katika mataifa yote; na Yerusalemu utakanyagwa na Mataifa, hata*... (Amina!)...*hata majira ya Mataifa yatakapotimia.*

74 La kugutua, sivyo, kujua kuwa tuna wakati mchache? Mungu alisema hivyo! Majira ya Mataifa yalianzishwa na Mfalme Nebukadreza. Ee, ajabu vipi! Ningetumia wakati kiasi gani kwa hili, kwa dakika chache tu! Lakini tazama, kila mtu ataka swali lake. Lakini, tukiwa kwa hili, hebu tufikirie hili, kwa sababu ni muhimu sana sasa, hivi *sasa*.

75 Tazama! Mungu aliwaongoza watu, Wayahudi. Hawakupata kuwa taifa, walikuwa tu watu. Nao hawakupata kuwa kanisa la kidhehebu, walikuwa tu *lile* kanisa lililoitwa. Hapakuwepo serikali miongoni mwa Wayahudi, kila mara wao waliongozwa na Mungu.

76 Ndipo wao walipotaka kuwa, kisiasa, kitaifa...kuwa na mfalme. Na Mungu akawapa mfalme na haikufaulu kamwe. Mungu ni Mfalme wao, Mungu ni Mfalme wetu, naam, na Mungu ni Mfalme wa Kanisa.

77 Sasa, tazama basi walipotekwa nyara na kuchukuliwa hadi Babeli kwa sababu walijaribu kuiga mataifa ya ulimwengu. Ni mfano mzuri jinsi gani siku hizi wa kanisa kujaribu kuiga ulimwengu nje kule, na kuchukuliwa mateka, kutekwa nyara kwa maisha ya—yao. Kanisa linaishi vivyo hivyo kama ulimwengu ufanyavyo, linatenda yasiyofaa, linatenda tu kama wao, na kadhalika, na kudai kuwa Kanisa. Huwezi kufanya hilo. La, bwana. Maisha yako yenyewe yathibitisha ulivyo.

78 Ulivyo. . . Kama nilivyosema mwanzoni, kile ulicho mahali penginepo ndicho uonyeshacho hapa. Wewe ulivyo, jinsi mwili wako wa kimbinguni au wa duniani ulivyo juu kule, jinsi mwili wako ulivyo mahali fulani ndivyo unavyoonyesha nyuma hapa. Katika nchi ya roho, jinsi ulivyo hapa. Kama ungali una nia chafu na mengineyo katika nchi ya roho, wewe u wa nia chafu hapa. Kama bado una wivu, husuda, na ubishi, uko na hayo katika nchi ya roho, inajionyesha hapa. Lakini kama utu wako wote wa ndani umetakaswa na kuoshwa, inaonyesha una mwili kule (unaongoja) ambao umetakaswa na kuoshwa, na umekuwa ukirejesha hayo katika mwili. Je, hamwoni? Ona, ndilo hilo. "Nyumba ya maskani yetu iliyo ya dunia hii ikiharibiwa, tunalo jingine tayari linalotungoja." Ona?

79 Sasa, katika wakati huu, wakati wa mwisho, jinsi huu mlingano wa kimwili, uigaji wote wa Ukristo utachanganyikana katika Babeli moja kuu kama ilivyofanyika nyuma kule. Nao wakachukuliwa hata Babeli. Sivyo? Na Biblia ilisema, "Malaika wa Bwana akapaza sauti na kusema, 'Tokeni Babeli, watu wangu!'"

80 Farakano! Hili, "Mimi ni Mbaptisti, mimi ni Methodisti. Mimi ni Mpresbiteria," hayo yote ni mafarakano. Hamna wokovu kamwe mle.

81 Sasa, usiseme kuwa ninasema Wabatisti hawana wokovu, Wamethodisti. Sineni kuhusu hilo. Mimi nanena kuhusu kanisa na nguvu zake za kisiasa, siasa zake. Na kunena kisiasa, kwa sababu wewe u Mmethodisti, wala Mbaptisti, wala Mpresbiteria, au Mkatoliki, halifai kitu. Mungu hata hayatambui na yamo katika Babeli siku hizi. Na Mungu anaita Kanisa toka kwayo yote, akiwatoa walio wasafi mioyoni, kufanya Kanisa Lake. Ni nzuri vipi!

82 Na tazama, ningesema jambo fulani hapa ambalo lingewashtua, lakini kama—kama ni. . . Sikiza, sasa. Tazama jinsi Babeli. . . Yaliyotendeka kule. . . Ba—Babeli waamini wa kweli walipodhulumiwa. Kumbuka, wacheche tu,. . . Shadraka, Mishaeli, na Abed—nego, na Danieli, wa—waabudu wa kweli walioenda utumwani, Mungu alipowaita ku—kuonyesha walivyo hasa, jinsi walivyokuwa. Walilazimishwa kuabudu sanamu. Sivyo? Ibada ya sanamu! Walilazimishwa kuabudu sanamu, nao

iliwabidi kusujudu mbele ya sanamu. Na kama hawakufanya hivyo, waliteswa.

83 Ee, ni mfano jinsi gani ungeutoa katika Danieli, Ufunuo, kufunganisha hayo yote pamoja na kuonyesha kwa Maandiko kuwa Kanisa litaingia katika mateso kama hayo kabla halijaondolewa. Hivyo ndivyo Kanisa la Mataifa lilivyoanzishwa, hivyo ndivyo Kanisa la Mataifa litakavyoondolewa. Jinsi lilivyoingia ndivyo litakavyoondoka.

84 Na tazama jinsi yeye alivyoona hiyo sanamu. Na sasa, kumbuka, ile sanamu . . . Naam, hapa ni nyumbani kwangu sasa. Tazama, naamini kuwa sanamu aliyofanya Mfalme Nebukadreza ilikuwa ya Danieli, mtu mtakatifu. Ukichunguza, mfalme Nebukadreza aliisha muita Danieli, alimwita "Belteshaza" (ambayo ilikuwa sanamu yake), naye akafanya—akafanya sanamu, na hakuna ye yote baada ya Danieli alikuwa ametupwa katika tundu la simba, na kadhalika, naye alisema, "Mtu ye yote asitumikie miungu mingine iwayo yote, na kadhalika, ila Mungu wa Danieli." Labda ilikuwa sanamu ya mtu mtakatifu, sanamu kuu, na kila mtu ilimbidi aisujudie hii.

85 Lakini Kanisa, Shadraka, na Mishaeli, na Abednego . . . Danieli akiwa kiongozi, kama Kristo alivyo Kiongozi wa Kanisa.

86 Na—iliwabidi wasujudie sanamu hii na kuabudu sanamu. Tazama! Nanyi mwatambua, katika siku hizo, Danieli alikuwa kimya. Amina! Ee, nami natumai mwapata hili. Danieli alikuwa kimya. Akiwaachilia wao . . . iliwapasa wajichagulie wenyewe.

87 Katika siku . . . majira ya Mataifa yatakapokwisha, kutakuwa na sanamu, na kila mtu itambidi asujudie mbele ya sanamu hii na kuabudu. Haidhuru ni takatifu vipi, haiwapasi kuabudu sanamu (ibada za sanamu).

88 Sasa, tazama. Jamani! Mwishoni kabisa, Danieli aingia tena. Ajabu vipi! Usiku huo, kabla ya ile karamu kubwa ya masuria na kadhalika, kukatokea Mkono ulioandika ukutani, "MENE, MENE, TEKELI, NA PERESI," ukutani kote. Na tafsiri yake, hakuna ye yote angetoa, yaliandikwa kwa lugha isiyojulikana. Hakuna ye yote angeitafsiri.

89 Walienda wakawaleta wanavyuoni wao walio bora sana. Wao wakasema, "Hatujui."

90 Walienda wakawaleta wachawi wao wote na wanajimu. "Hatujui. Hatujui lo lote kuhusu Hayo. Hatujawahi kuona lugha hiyo, hatujawahi kusikia mambo kama hayo maishani mwetu."

91 Lakini kulikuweko mtu! Mungu alikuwa na mtu Wake, Danieli alikuweko. Kasema, "Nendeni mkalete," kasema, "kwa kuwa Roho ya Mungu huishi ndani yake."

92 Kwa hivyo Danieli akaja pale, akaanza kusoma na kutafsiri hiyo lugha kwenye ukuta, naye akatoa . . . Tafsiri ilikuwa nini? Si

"Ee, umebarikiwa, Ewe mfalme, ishi milele." Lakini akimkataa wazi-wazi na kwa ushupavu kabisa, kasema, "Umepimwa kwenye mizani nawe umeonekana kuwa umepunguka."

93 Tazama, ni vivyo hivyo. Kama vile ya Kimbinguni yalivyoanzisha ufalme wa Mataifa, ndivyo ya Kimbinguni yanavyoondoa huu wa Mataifa. Ufalme ule ulitanguliwa na ya Kimbinguni, unaondoka kwa ya Kimbinguni. Zile kuta za Yerusalemu zitakanyagwa, na zitakuwa. . . zingekuwa . . . "Mataifa wataushikilia hata majira ya mataifa yatakapotimia." Ndipo Mungu atawarudia Wayahudi. Amina! Jamani!

94 Ee, marafiki, natumai tungelipata hilo vizuri. Sivyo? Tuwe na karibu juma moja kwa hilo somo moja, ona, ili tulichunguze kweli kweli Maandikoni.

95 Hilo, tazama, sikiza—sikiza kwa makini sasa Yeye alivyosema, "Yerusalemu itakanyagwa na Mataifa hata majira ya Mataifa yatakapotimia." Kuzingirwa na—na Tito, ndipo akaingia, akauteka Yerusalemu. Yeye alisema, "Naam—naam, mlisikia kuhusu lile chukizo la uharibifu?"

"Naam."

"Vema, hapo ndipo Mataifa yalipoingia."

"Naam, twafahamu hilo," wakasema wanafunzi.

"Basi, Mataifa wamekwisha kuwa na serikali yao."

"Bila shaka."

96 "Yerusalemu chini ya serikali ya Mataifa?" Naam, bwana! Wale Warumi. Walikuwa wangali wanatawala Ye—Yerusalemu. Na ilianza nyuma kule kwa lile chukizo la uharibifu Danieli alilonena.

97 Basi Yeye akasema, "Wakati huo umekaribia, kwa kuwa watalivunja hekalu hili na wajenge Uislamu wa Omar, utasimama mahali papa hapa, wale Waislamu, Mataifa. Na litasimama pale."

98 *Mataifa* maana yake ni "wasioamini." Hilo halikuwa Kanisa, sasa. Hilo lilikuwa Mataifa, ona, wasioamini. Sasa, na hilo litasimama hata majira ya Mataifa yatakapotimia. Ndipo majira ya Mataifa yatakapotimia, yule Mtawala mkuu atawapigania watu (Ambaye ni Kristo) wakati wa mwisho.

99 "Yeye akamkaribia Yeye," katika Danieli, "Yeye yule nywele Zake zilikuwa nyeupe kama sufu," jinsi mnavyomwona katika Ufunuo 1, "kwa yule mzee wa siku. Na hukumu Ukawekwa na Vitabu vilifunuliwa. Vitabu," (wingi) "vilifunuliwa na kila mtu alihukumiwa kulingana na Vitabu vile, katika mambo hayo yaliyoandikwa humo." Tazama, Vitabu vilifunuliwa, "Yeye alimwona Yeye akija, na kumi ya maelfu mara kumi ya maelfu walimhudumia." Watakatifu walikuja pamoja Naye. Sivyo, katika Danieli? "Na Vitabu vilifunuliwa," hicho ni kile

Kitabu cha Uzima, "na kila mtu—na kila mtu alihukumiwa hivyo, mwenye dhambi, alihukumiwa hivyo. Na Kitabu kingine kikafunuliwa," ambacho ni Kitabu cha Uzima, "na kila mtu alihukuniwa."

100 Sasa tazama, kila wakati kumbuka, ibebe katika utatu. Usipofanya hivyo, bila shaka itakutatiza. Kulikuwa na tabaka tatu za watu waliozaliwa duniani; kulikuwa na tabaka tatu mwanzoni, kutakuwa na tabaka tatu mwishoni. Kile . . .

101 Yesu alirudi pamoja na kumi ya maelfu mara kumi ya maelfu waliomhudumia Mwakumbuka aliposema, "Je, si jambo ndogo kwenu kuchukua . . . au jambo lisilo la kawaida kupeleka shughuli zenu na shida zenu kwenye sheria, hamjui kwamba Watakatifu watahukumu ulimwengu?" Watakatifu kuhukumu ulimwengu! Haleluya! Nawaza hilo, jamani! Kumwona Yeye akija, huko ng'ambo pamoja na wale waliooshwa kwa Damu, baada ya ule Utawala wa Miaka Elfu, ukombozi na waliokombolewa wa nyakati zote wamesimama katika Uwepo Wake, Yule Bibi-arusi aliyeoshwa kwa Damu.

102 Si eti wale walio wema tu, hao bila shaka hawatashiriki ule ufufuo wa kwanza. Biblia ilisema, "Hao wafu waliosalia hawakufufuka hata itimie ile miaka elfu." Sivyo? Hao ni wale ambao majina yao yalikuwa kwenye kile kitabu cha Mwana-Kondoo cha Uzima bali walikataa ubatizo wa Roho Mtakatifu.

103 Wateule pekee wanaingia wakati huo. Wateule pekee watashiriki U—U—Utawala wa Miaka Elfu. Ee, basi, ndugu, twapaswa kuwa watu wa namna gani? Nataka niishi katika huo Utawala wa Miaka Elfu wote! Na tuweke kando kila mzigo mzito na dhambi ile ituzingayo kwa upesi. Mtu fulani akisema kitu fulani kibaya au akifanya hivi, mwombee na ushike njia. Na lengo lako liwe Mungu. Kama hakuna mwingine atakayefaulu, wewe faulu! Kwa kuwa kutakuweko Wateule watakaoishi kwenye huo wakati wa Utawala wa Miaka Elfu na wataingia na kutoka pamoja na Kristo kwa miaka elfu, ndiposa wataenda juu Utukufuni Pamoja Naye na kurudi tena. Ufufuo wa walio waovu ujapo, ndipo ule Utawala wa Miaka Elfu utakapoanza . . . Baada ya huo Utawala wa Miaka Elfu, ndipo Kristo atakapopaa juu pamoja na Kanisa, na mwishoni mwa ile miaka elfu Yeye atarudi pamoja na Kanisa.

104 Kristo yuaja mara tatu. Mara ya kwanza Yeye alikuja *kukomboa* Kanisa Lake. Sivyo? Mara ya pili, Yeye yuaja *kupokea* Kanisa Lake. Mara ya tatu Yeye yuaja *pamoja na Kanisa Lake*. Ona? Yeye yuaja *kulikomboa*; Yeye yuaja *kulinyakua* na kulichukua, katika siku za yale mapigo na kadhalika; arudi tena kwa ajili ya ule *Utawala wa Miaka Elfu,* aishi katika wakati ule wote wa Utawala wa Miaka Elfu.

105 Na ndipo yule Mfalme mkuu na Malkia wanashuka kwa ajili ya Hukumu. Ule Hukumu wa kile kiti Cheupe cha Enzi

utaanza na vitabu vikafunguliwa. Ndio hao waliokombolewa, Kanisa lililozaliwa na Roho Mtakatifu la Mungu aishiye, likisimama pale katika uzuri Wake kuhukumu. "Vitabu vile vilifunguliwa, hukumu ikawekwa na kila mtu akahukumiwa kulingana navyo," huyo alikuwa mwenye dhambi. "Na Kitabu kingine kilifunguliwa," si kwa ajili ya Bibi-arusi aliyejazwa na Roho Mtakatifu, yeye hatahukumiwa kamwe kwa sababu Yeye amekwisha kunyakuliwa.

106 Kama umejazwa Roho Mtakatifu asubuhi hii, na nguvu za Mungu zinatembea katika kila mshipa wa mwili wako, ingalikufaa nini kusimama Hukumuni? Wewe umekwisha kuhukumiwa, na umepokewa, na kujazwa, na umekwisha— umekwisha inuliwa katika ulimwengu wa Roho pamoja na Kristo Yesu. Si kuwa *utakuwa*, bali umeshakuwa sasa, hivi sasa umekwisha kugeuzwa!

107 "Wale aliowaita, aliisha wahesabia haki, wale aliowahesabia haki, amekwisha kuwatukuza." Na kila mtu aliyekombolewa ulimwenguni asubuhi hii, aliye chini ya Damu ya Yesu Kristo, amekwisha kujazwa na Roho Mtakatifu, *yuna* Uzima wa milele na hataangamia, na tayari yumo katika ulimwengu wa Roho katika Kristo Yesu, na hatahukumiwa kamwe. Amekwisha kukombolewa! Si hilo ni la ajabu? Ona? Amekwisha kombolewa, anaketi katika ulimwengu wa Roho sasa pamoja na Kristo, na kutuku . . . amekwisha kutukuzwa, amekwisha kutukuzwa!

108 Unasema, "Ndugu Bill, Je, Maandiko yasema hayo?"

109 Yesu alisema hayo, au Maandiko yanasema hayo, au waandishi. Paulo, alisema, "Wale aliowahesabia haki, hao akawatukuza. Wale aliowachagua tangu asili, hao akawateua tangu asili; wale aliowateua tangu asili, hao akahesabia haki, wale aliowahesabia haki, amekwisha kuwatukuza." Ni nini? Jamani! (kunradhi) Wamekwishatukuzwa! Ndipo kama tumejazwa na Roho Mtakatifu, miili yetu na utu wetu vimekwisha hifadhiwa na Mungu, ule mwili uliotukuzwa tayari unangoja, nawe huna budi kwenda Kwake mara tu huu uishapo. Wale aliowahesabia haki, hao amekwisha kuwatukuza!

110 Nilivyokuwa nikisema muda mchache uliopita, kivuli na kitu halisi. Laiti ningalikuwa na elimu ya kutosha kuyaeleza hayo na kuyafanya wazi na dhahiri kwenu, lakini sina. Najua yale ninayonena, lakini siwezi kuyaeleza nitakavyo.

111 [Nafasi tupu kwenye ukanda—Mh.] . . . Bahari ya Shamu na vitu hivi vyote wanavyoweka mashambani mle, Wayahudi, vya thamani sana, ndipo kitu kile kile kitachafua makao yao tena. Naam! Watakuja toka kote, miji ya ulimwengu. Urusi itakuja, iseme, "Lazima tunyakue kitu hicho. Hicho ni yale madini ya uranium na vyo vyote vile chini kule, hatuna budi kwenda kuvinyakua." Nao waendapo chini kule, ndipo vitazuka vile Vita vya Amagedoni. Hapo ndipo Mungu atakaposimama

jinsi alivyosimama katika lile bonde kwa ajili ya wana wa Israeli na kupigana tena. Lakini hayo yatatendeka hata majira yatakapotimia. Na wakati huo utimiapo, watakatiliwa mbali.

112 [Nafasi tupu kwenye ukanda—Mh.] Sasa, maoni yangu manyonge, mtu mpendwa—uliyeuliza swali hili hapa, nionavyo mimi kuhusu hili.

10. Hawa wanefuli walikuwa akina nani siku hizo?

113 Sasa, Josephus pale . . . Bila shaka, najua kanisa letu, mko tu kama mimi. Mimi—mimi ni mtu duni wa darasa la saba na—nami sijali elimu na kadhalika. Nadhani ndiyo kizuizi kikubwa sana Injili ilichowahi kuwa nacho. Ingawaje, mara kwa mara tu, nachukua kitabu kimoja viwili. Sasa, uhusiano wangu na watu kama mimi mwenyewe, sisi sote ni sawa, sisi ni watu wa kawaida tu. Nami nashukuru sana Biblia ilisema, "Watu wa kawaida walimsikiza kwa furaha." Wale matajiri, halafu kulikuwako na kundi lingine, lakini watu wa kawaida . . . Wananchi wa kawaida tu kama tulivyo sisi, watu wampendao Mungu na ambao hawana mengi ya ulimwengu huu, wana watoto wao na jamaa zao, twampenda Mungu na twapenda kuenda kanisani, kutoa ngu—nguo zetu kwa ajili ya Ufalme Wake, cho chote kama hicho. Twampenda Yeye, tutafanya cho chote, hao ndio watu wa kawaida waliomsikia. Na ingali vivyo hivyo leo, watu wa kawaida walimsikiza kwa furaha.

114 Sasa, tajiri ana mambo mengi sana ya kidunia ya kufikiria, ona. Na—na mtu halisi chini pale ambaye huwezi kufanya cho chote naye, kwenye vitongoji vya mji, yeye hatajali haya kamwe. Lakini watu tu wa kawaida walimsikiza kwa furaha.

115 Na sasa katika Josephus, maandishi yake, alisema . . . Naam, hii ndiyo tafsiri yake ya hawa "wana wa Mungu" waliojitwalia binti za watu. Yeye alisema kwamba "Zile roho zilizoanguka zilizokuwa duniani . . . "

116 Sasa, mwajua . . . katika Ufunuo, sura ya 11 . . . au ya 7, la, samahani . . . sura ya 12 ya Ufunuo, yule mwanamke aliyesimama katika jua. "Lile joka kubwa jekundu lilifungia mkia wake theluthi mbili ya nyota na kuziangusha duniani." Twatambua kuwa Shetani, mwanzoni, alianzisha ufalme katika nchi za kaskazini awe mrembo zaidi kuliko vile—kuliko Mikaeli alivyokuwa, na siku moja yeye akatangaza vita Mbinguni. Naye akakokota theluthi mbili ya viumbe vya kimalaika. Sivyo?

117 Hiyo ndiyo sababu sisi ni wachache tu. Nakusudia u—u—u uchache . . . uchache wa watu asubuhi hii, katika mazingira ya Kikristo, watu waliozaliwa na Roho Mtakatifu, kwa sababu wao ni—ni—ni wachache. Naam.

118 Na ukichunguza zile roho zilizotoka Mwanzo na kuanza kuinuka, tazama hizo ibada za kielimu sana, ibada bora na za hali ya juu sana. Zitazame nyuma kule katika Kaini, zitazame siku hizi. Zikaja moja kwa moja hata zikaingia katika

Mafarisayo. Na kuna madhehebu mawili yazo, Mafarisayo na Masadukayo, ona, zikatoka pale na kuendelea, na zitazame siku hizi katika—Ukatoliki na madhehebu makuu kama hayo, majengo makubwa na mazuri.

119 Vema, mtazame Habili na mwana-kondoo mdogo, ona, wa kawaida. Itazame katika siku za Yesu. Itazame kote Maandikoni unapoifuatilia, kuona jinsi ilivyo. Tunaishi papo hapo katika siku ambayo Mungu ameliita kanisa Lake kote kote. Huo mwali mdogo, huo mwali mdogo mwekundu uliopenyeza kote kote katika Biblia, kote, wa watu waliooshwa kwa Damu. Tazama!

120 Sasa, hawa "wana wa Mungu," kwa maoni yangu, bila shaka huenda . . . Si kumpinga au kujaribu kujifanya mwerevu au kusema kuwa Josephus hakujua aliyokuwa akinena, lakini yeye alikuwa mwanadamu kama nilivyo mimi. Haidhuru alikuwa mwanachuoni jinsi gani, yeye ni mwanadamu. Na jambo pekee yeye alilofanya, alichunguza maandiko ya kale, na kadhalika, zile kumbukumbu za kale, na kadhalika, lakini hakuwa na zaidi ya kile tulicho nacho siku hizi, Roho Mtakatifu. Naam, alitegemea tu akili ya kawaida.

121 Lakini sisi tunategemea mawazo ya kiroho, wale "wana wa Mungu," kusema kuwa walikuwa viumbe vya kimalaika. Naamini walikuwa hivyo. Na—nami naamini kwamba hao . . .

122 Naam, Josephus alisema jambo lile lile, lakini yeye alisema, "Walijisukumiza na kujipenyeza wenyewe katika miili ya wanadamu, na kutwaa wana . . . na—na kujitwalia binti za wanadamu." Sasa, sisi ni kundi lililochanganyikana; sisi ni mchanganyiko hapa asubuhi hii, wanaume, wanawake, na wasichana na wavulana wadogo, nami nanena hili ili watu walifahamu kabisa. Lakini wakati . . . Yeye asema kwamba "Wakati viumbe wale wa kimalaika walipoona tamaa ya wanawake, jinsi wanaume walivyoishi na wanawake, kuwa wao walijisukumiza katika miili ya binadamu. Kwa hivyo . . . nao wakajitwalia wenyewe binti za wanadamu."

123 Vema, si—siamini hilo. Naamini hili, kuwa walizaliwa kule Kanani, nao walizaliwa kwa—kwa lile—lile kundi la Kaini lililofukuzwa kwenda nchi ya Nodi. Naye alikuwa na alama kwamba mtu ye yote asimuue, kwa sababu ya mauaji yake . . . ni marufuku, yeye alimuua ndugu yake. Lakini kama, unaoana, hata Waisraeli waliwakuta baadhi ya watu hao walipoenda kule. Walikuwa wakubwa sana, nao walisema walionekana kama panzi, kando yao. Sivyo? Mamia na mamia ya miaka baadaye, kulikuwa na watu wakubwa na wanene, watu wakubwa mno. Na wakati mwingine wao huchimbua mi—mizoga yao, nao waliona kuwa wao walikuwa watu wakubwa.

124 Sasa ninakowaza walitoka. Naam haya ni mafundisho yangu madogo sasa. Ni kwa watu wa kanisa tu, ona. Nadhani Kaini alikuwa mwana wa Shetani. Najua hamkubaliana na

hilo, kanisa langu lakubali. Lakini hilo bado . . . Hadi Mungu anionyeshe vinginevyo, ni—nitaamini jambo lile lile, ona, kuwa yeye alikuwa mwana wa Shetani. Kwa kuwa singekubali kwamba huyo roho asiyemcha Mungu, muuaji, kwamba anatoka kwa Mungu. La, bwana. Yeye alipaswa kuwa mfano wa baba yake na alikuwa huyu . . . hapa, Shetani alipomwingia yule nyoka.

125 Na nyoka huyo hakuwa mnyama mtambaazi, laana ilimfanya awe mnyama mtambaazi. Yeye alikuwa tu kama mwanadamu, alitembea wima. Naye akaenda na mwanamke huyu nje kule, kisha akazini na kujizalia mwanawe wa kwanza ambaye alikuwa Kaini, tabia ya baba yake. Nami naamini huyo mnyama mkubwa alisimama wima kama mwanadamu, naye alitembea wima, na hapo ndipo hawa wanefuli wakubwa walitokea. Naam, ndivyo hasa. Sasa, hayo ni maoni yangu na—nami naweza kukosea. Hayo ni maoni yangu, ona. Lakini walikuwa watu wakubwa mno.

126 Na ukichunguza, Mungu akisimama pale mbele ya Adamu na Hawa, Yeye asema, "Niliwatwaa mavumbini, mtarudi mavumbini. Mimi . . . "

127 "Na kwa sababu umeleta . . . ulimsikiza . . . huyo mnyama badala ya mume wako, hata ukapata uhai kutoka nchini, wewe utaurudisha tena nchini."

128 Na Yeye alisema, "Nyoka, miguu yako iondoke, ona, hutatembea wima tena. Na hutakuwa mnyama tena, utakuwa mnyama mtambaazi sasa. Na utatambaa kwa tumbo lako, na mavumbi yatakuwa chakula chako."

129 Pale ndipo ninapodhani kuwa hao . . . Kaini, akichukua umbo la huyo fidhuli aliyeishi na . . . kama mnyama, aliyeishi na mwanamke huyo aliyemzaa mtoto huyu, ambaye alikuwa nusu mnyama nusu mwanadamu, mtu mkubwa mno. Ndiposa yeye alienda nje kule na watoto wake wakaanza kuzaliwa kwake, ndiposa hao wanyama, wenye tamaa ya zinaa kama baba yao hapo mwanzo, maskini tamaa hizi mbovu za kinyama zikawapata binti hawa na mengineyo, na kujitwalia binti za wanadamu. Naam.

130 Na kilichowaingilia hawa watu, bila shaka, kiliendelea moja kwa moja katika ukoo uo huo ambao ulikuwa roho zilizoanguka zilizowapagaa watu wale. Kumbuka, roho zile zile zilizoishi nyuma kule, leo . . . zinaishi leo.

131 Itazame siku hizi! Vema, tunao watu nchini humu ambao . . . Sasa, mimi si . . . Hili, mimi ni Mwamerika, mwajua hivyo. Lakini hebu niwaambieni, hili ndilo taifa duni sana mbali na Paris, Ufaransa, nilijualo po pote ulimwenguni. Limepotoka kabisa!

132 Naam, hata watu wa nchi za kigeni, katika Afrika, katika—katika Sweden na . . . juu kule, wao husema, "Vipi ninyi watu wa Amerika, je, hamna heshima tena kwa wanawake wenu? Kwa

ajili ya nyimbo hizi redioni, chafu sana, nyimbo zinifu kuhusu wanawake. Je, hamwaheshimu wanawake wenu kule?"

133 Nyimbo zetu zote zinahusu wanawake, au zinaa na tamaa mbovu, na mambo kama hayo. Ni kwa sababu Shetani amelikumba. Naam hasa. Hollywood ya kale na matelevisheni na kadhalika zinaeneza huo ushenzi na mambo yasiyomcha Mungu, watafikia hata viwango vipya na kadhalika. Kila kitu ni wanawake uchi au cho chote kile. Hivyo ndivyo ilivyoanza hapo mwanzo, na itaishia vivyo hivyo. Ni aibu!

134 Na uti wa taifa lo lote ni uwanawake, tukinena kuhusu uadilifu. Na unapovunja umama, umevunja taifa lako. Tumefikia mahali siku hizi ambapo hata wanawake wetu . . . kuvuta sigara, na mambo kama hayo, na kunywa mvinyo, na kuendelea, na ni—ni aibu!

135 Kijana mwanamume kujaribu kumpata mwanamke ambaye hata ni bikira, aliye mwadilifu, itambidi aende kwenye kanisa zuri lenye Roho Mtakatifu, ndogo, la kale, ampate mmoja, kwa shida; na hiyo ni kweli hasa, ambapo mtu fulani alimfungia ndani na mambo kama hayo, hata akapata uadilifu mdogo.

136 Huenda ukadhani hilo ni kichaa, lakini ndugu, chunguza utaona, uone kama hilo si Kweli. Ni aibu! Vema.

Wao walikuwa wale wana wa Mungu walio . . . Sasa, hilo, naweza kueleza . . . Ona, nami najua niki . . .

137 Nilikuwa na swali lingine, wao husema, "Naam, Ndugu Bill, Biblia ilisema Hawa alisema, 'Nimepata mtoto mwanamume kwa Bwana.' Bila shaka. Ilibidi aje toka kwa Bwana. Bwana ndiye Muumba pekee. Yeye . . . Mungu alimuumba Shetani. Na hilo je? Mungu alimuumba shetani. Mungu alimuumba kila malaika aliyeanguka aliye hai. Sivyo? Naam, Bila shaka. Hilo lilikuwa chaguo lao, si Lake. Yeye alikuumba wewe, unafanyaje kuhusu hilo? Utahukumiwa vivyo hivyo kama wao. Naam. Bila shaka!

138 Hawa walikuwa wana wa Mungu, bali walikuwa wameanguka toka kwa neema na walikuwa wameingia katika huyu mtu wa kinyama, na kukimbia nje na tamaa mbovu. Walipowaona wanawake, wakawashika tu. Naam, bado wangali hapa. Utovu wa uadilifu wa Amerika umejaa—wanaume wasio na Roho wa Mungu, wangemtupa mtoto mchanga toka mikononi mwa mamaye na kumnajisi huyo mama. Bila Mungu, yeye si—yeye si bora kuliko mnyama. Yeye bado anayo hiyo tabia ya mnyama, isiyomcha Mungu. Na mtu aliye na . . . Wao husema, "Dini ina ladha nzuri, kwa hivyo wanadamu wameipenda sana dini. "Dini ndicho kitu pekee kiwezacho kumpa mtu akili zake timamu, hiyo ni kusema, dini ya Yesu Kristo.

139 Ningethibitisha kwa Biblia kuwa wewe huna akili timamu hata utakapompokea Kristo. Naam. Hilo ni nzito sana, lakini naweza kuthibitisha kwa Maandiko. Naam. Unakuwa mnyama,

mwenye tamaa mbovu na kadhalika hata utakapompokea Kristo Yesu. Yeye ndiye Mtu apendezaye.

140 Sasa, nitakubali kuwa watu husoma kupita kiasi, na kujaribu kuenda mbele kupita kiasi, kujaribu kutafakari mno, na wakati mwingine hurukwa na akili na kadhalika kwa kusoma mno habari za Bwana. Yakubidi uache hilo! Haikupasi kufanya hivyo. Jambo pekee likupasalo kufanya ni kupendana Naye, na kuendelea tu kumpenda Yeye. Naam. Si kujaribu kujisukumiza katika kitu fulani au kujifanya mwenyewe kitu fulani usichokuwa, endelea tu na acha Mungu akutumie katika njia atakayo. Jitolee nafsi yako, jikabidhi mwenyewe na endelea, mwenye furaha, anayeimba, anayeshangilia. Hivyo ndivyo ipasavyo.

141 Biblia ilisema, "Katika mambo yote Mungu hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema," kwa hivyo hakikisha ya kwamba unampenda Yeye, hilo ndilo jambo pekee likupasalo kujua. Amina! Mpende tu na uendelee! Usema, "Bwana, nakupenda, wajua nakupenda."

"Unapenda *hili?"*

"La, bwana. Nakupenda, Bwana." Ona?

142 Sema, "Vema, hutaki ku. . . Hungependa kuwa mhubiri mkuu? Hungependa kuwa *hivi?"*

143 "La, sasa, Bwana, nini. . . Ukitaka niwe, nitakuwa. Usiponitaka niwe, Amina. Nitakuwa papa hapa, zulia tu hapa kanisani."

144 Vema, sasa naamini ukifanya kitu fulani kama *hiki* watu watalipenda kanisa lako zaidi."

145 Sijui wanavyodhania, nataka nijue wewe unavyonidhania, Bwana. Ni—nitakaa pamoja nawe, uniambiacho kufanya. Nawapenda wote, bila shaka."

"Vema, sasa, wajua Dada *fulani* humpendi."

"Naam, nampenda, Bwana. Naam, hakika nampenda. Nampenda."

"Mbona?"

146 "Kwa kuwa Wewe wampenda, Nawe uko ndani yangu. Nami sina budi kumpenda, kwa sababu ni Wewe uliye ndani yangu unayempenda." Whiu! Hilo litafaulu.

147 Lakini nadhani kuwa hao ni wale wanyama walioanguka mle, wale, wale. . . ?. . . wanyama walioanguka, ona.

11. Je, "wana wa Mungu," lamaanisha Malaika au roho kutoka Mbinguni?

148 Hilo lilikuwa swali la huyo mtu. Vema. Naamini kuwa hawakuwa Malaika. Ona, walikuwa viumbe, "wana wa Mungu," kama Maandiko yasemavyo, si malaika, wao walikuwa wana wa Mungu. Wao walitoka Mbinguni kuja duniani, na wakawekwa

katika mwili, hawakujisukumiza nafsi zao katika miili," naamini miili yote inazaliwa kwa kujuana kimwili isipokuwa wa Yesu Kristo. Naamini Yeye pekee ndiye kiumbe aliyewahi kuzaliwa na bikira, Yesu Kristo. Nami—sikubaliani na Josephus kuhusu hilo, ijapokuwa yeye ni mwanahistoria mkuu. Lakini naamini kuwa wao ni viumbe vya kimbinguni vilivyoshuka na kutawala roho za watu. Nami naamini bado wako papa hapa siku hizi, bado wanatembea hapa na pale Jeffersonville leo, zile roho za kinyama, zenye tamaa mbovu, zisizomcha Mungu, kuishi katika wanadamu. Sasa, siku moja watu hawa watakufa; na kama kuna kizazi kingine, zitawajilia juu yao.

149 Kumbuka, Mungu humtwaa mtu Wake ila si Roho Wake, huyu ni Roho Mtakatifu yule yule waliyempokea kwenye siku ya Pentekoste.

150 Ni Shetani yule yule (katika hali za kidini) aliyemtesa Kristo, ni Shetani yule yule aliye kanisani siku hizi, amevalia majoho marefu. Na haiwapasi kuvalia . . . Sisemi majoho juu ya miili yao, nasema majoho juu ya nafsi zenu. Ona, "Naam, siku za miujiza zimepita, hakuna kitu kama hicho." Nena kuhusu Mafarisayo mamboleo! Vivyo hivyo.

151 Hata hivyo, Biblia ilisema, "Watakuwa na mfano wa utauwa, bali wakikana Nguvu zake. Hao nao ujiepushe nao, achana nayo. Usiyakaribie, usiyaendee." Wangali wana wa Mungu, bali wangali wameanguka. Mwaona ninalomaanisha? Wengine wao ni wahudumu, wengine wao ni mashemasi, wengine wao ni wazee, wengine wao ni maaskofu, wasafi kweli kweli! Lakini Biblia . . .

152 Sasa, nitajibu lile swali, ndugu, ulilouliza muda mchache uliopita. Mtu fulani alisema:

12. Ndugu Branham, nataka kujua mahali amba ambapo naweza kushikilia na kusema, "Mwanamume huyu ana Roho Mtakatifu kwa sababu yeye alifanya "hili, au "Mwanamke huyu ana Roho Mtakatifu kwa sababu yeye alifanya "hilo".

153 Hakuna njia kamwe kwako kujua hilo. Naam. Hakuna njia kamwe uwezayo kujua hilo kwayo. Mungu ndiye hakimu, sisi hatupaswi kuhukumu. Ona? Hubiri Injili tu, ishi . . .

154 Mtu fulani alinijia wakati fulani uliopita, nilikuwa nikihubiri kuhusu yale niliyosema usiku uliopita. Yeye alikuja hadi nyumbani kwangu na kusema, "Ndugu Branham, ndugu, nataka—nataka—nilitaka kuwa . . . nataka kuacha dhambi zangu. Nataka kuwa Mkristo." Yeye aliketi sebuleni mwangu.

155 Akasema, "Nalisikia kuhusu mtu mmoja mashuhuri, mtu anayejulikana duniani kote aitwaye Billy Granham." Alisema, "Nilihudhuria mikutano yake na—na naye alisema, 'Wote wanaotaka kuwa Wakristo, inueni mikono yenu na mkubalini Kristo kama Mwokozi wenu binafsi.' Kwa hivyo nikauinua

mkono wangu. Akasema, 'Sasa, nyote simameni, tutaomba.' Kwa hivyo nikabaki na kuomba tu . . . " (samahani) "kwa unyofu tu kadiri nilivyoweza." Akasema, "Na, lakini halikunifaidia kitu."

156 Akasema, "Ndipo nalishuka kwenda kwenye—kwenye mikutano ya Oral Roberts. Yeye akasema, "Nilisikia habari zake, nami nilisikia wote walikuwa na furaha kuu." Kasema, "Nalimwendea Oral Roberts na kumuuliza, "Nifanyeje nipate kuwa Mkristo?" Yeye akaniambia "Rudi ndani mle . . . " Nilimwambia nilikuwa nimeuinua mkono wangu katika mkutano wa Billy Granham. Yeye akasema, "Wewe keti katika hicho chumba cha maulizo ndani mle hata utakapokuwa na furaha sana na ukanene kwa lugha." Yeye alisema, "Niliingia ndani mle nami niliomba hata nikanena kwa lugha." Kasema, "Ikaja, lakini haikunifaidia kitu."

157 Yeye alisema, "Na ndipo nilienda kwa mkutano mwingine nao waliniambia nilikuwa bado sijatakaswa, kasema, 'Yanipasa nitakaswe na nipate furaha na kupiga shangwe, nipate furaha ya kutosha.' Kwa hivyo niliomba na kuomba hadi ni—nikapiga shangwe, lakini bado . . . "

158 Nilisema, "Ndugu, kila mojawapo wa mambo haya ni sahihi, kila majawapo ni mazuri. Kuinua mkono wako, kunena kwa lugha, kupiga shangwe, naamini kila mojawayo, bali hayo siyo kitu kile. Ona, ni kumkubali Mtu, Yesu Kristo." Ona? Ona, si ku.

159 Vitu hivi ni matokeo yake. Kupiga shangwe, kunena kwa lugha, kukimbia, kushangilia, kulia, kuomba, kupayuka, hivyo ni matokeo yanayofuatia. Jambo la kwanza ni kumkubali huyu Mtu, Kristo Yesu. Ona? Kwa hivyo hakuna—hakuna dhihirisho tunaloweza kutaja. Kwa sababu mtu hulia? Nimewaona watu wakilia na kulia, na kulia machonzi ya kinafiki, naye yuangali ni mwenye dhambi mkuu kweli kweli.

160 Sikiza, Yesu ana kondoo pekee. Sivyo? Mchungaji ajua kondoo zake. Kuna mtu ndani humu aliyewahi kusikia mbuzi akilia? Vema, ndugu, heri uwe mchungaji ukitaka kujua tofauti. Mbuzi atalia kama tu kondoo. Enhee. Acha na beberu ashikwe mahali fulani pale, na kondoo mdogo upande mwingine. "Baa," kisha "baa," vivyo hivyo.

161 Nami nimesikia wao chini kule madhabahuni wa—wakilia na kulia, "Ee, Mungu!" wakilia tu hivyo, "Ee Mungu!" na wao ni mbuzi daima. Naam, kupiga shangwe? Vema, lo, nimewaona wao wakipiga shangwe hata wana . . . nao hukimbia sakafuni na kuruka juu chini na kupiga shangwe.

162 Sasa, unasema, "Ndugu Branham, huamini katika kulia!"

163 Usinichukue kwa kosa. Bila shaka, naamini katika kulia. Lakini nasema hiyo siyo ishara, ona, kwa sababu wao wote wawili hulia. Nimeaona wao wakipiga shangwe kwa nguvu tu kadiri walivyoweza kupiga shangwe. Naam, bwana. Na wakiendelea tu hivyo. Na kuna wengi wao kati yenu, kile

ninachonena. Nimewasikia wakinena kwa lugha, wakiondoka na kuishi maisha yo yote, wakifanya tu cho chote. Kwa hivyo, hiyo siyo ishara.

Bali unasema, "Wewe unakupinga."

164 Lo, la. Naamini katika kunena kwa lugha, ni karama ya Mungu kanisani. Kama ningeiondoa, ningeondoa sehemu ya Mungu. Nikiondoa ulimi wangu—ulimi wangu mwilini mwangu hapa, singekuwa na mwili uliokamilika. Mwili wa Yesu Kristo una ndimi ndani Yake. Mwili wa Yesu hapa una ndimi; na ukiziondoa, unaondoa sehemu ya Kristo. Lakini huwezi kusema hizo ndizo Mwili, ona. Ona? Ona?

165 Lakini ni kumkubali Mtu, Kristo Yesu, na mambo haya mengine yanaingia moja kwa moja na kupatana. Na kila mshiriki katika mwili huu asubuhi hii, na hili kundi ndogo la watu, kama tungefungua pazia hizi pande zote na kila mtu ndani humu ampokee Mtu, Kristo Yesu, hakungekuwa na mzozo kamwe au hakungekuwa na ubishi. Kungekuwa tu na upendo mkamilifu. Bali mngali mnaamini *hili* na kuamini *hilo*, lakini upendo ungalijaa na . . . Ona? Naam. Sasa, Yesu alisema, "Kwa tunda lao mtawatambua." Na tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, wema, upole, utulivu.

166 Sasa, ninaenda ku . . . Nitawapa makadirio yangu ya yale nadhani kuwa ndiyo yanayokaribia sana ishara, ya kwamba mtu ni Mkristo, kuliko cho chote nikijuacho. Mwajua ni nini? Ni utungu wa nafsi. Mtu ambaye kila mara ana njaa na kiu cha Mungu. Wao . . . mchana na usiku, wao—wao hawawezi kujizuia. Yawapasa wamtendee Mungu jambo fulani. Wa—wamejawa na upendo nao . . . utungu wa nafsi zao, kuwa na utungu wakati wote. Biblia ilisema, "Yeye aendaye akipanda kwa machozi hakika atarudi tena, kwa kelele za furaha, aichukuapo miganda yake ya thamani." Sivyo? Mambo hayo yote.

167 Sasa, tazama, kuna . . . Kama kanisa hili . . . Kama ningesema, asubuhi hii, kuwa mimi pamoja na kundi hili la watu hapa . . . Na Mungu asema, "Sasa, tazama, William Branham, utajibu kwa niaba ya kundi hilo la watu, yale unayowaambia. Sasa, unawataka wote wapige shangwe?"

"Hakika, nawataka wapige shangwe."

"Unawata wote wanene kwa lugha?"

"Nataka kila mmoja wao afanye hivyo."

"Unawata wote wacheze katika Roho?"

"Na nataka kila mmoja afanye hivyo."

168 "Vema, sawa, hilo ni zuri, lakini ungetaka wafanye nini badala yake?" Enhee.

169 "Heri niwe na kanisa ambalo lilikuwa na mzigo sana mioyoni mwao wa maombi hata walikaa tu madhabahuni hapa na

wangekuwa hapa mchana na usiku, na kadhalika; na nyumbani kwao, waliomba daima, nao wanyenyekevu, huku wakijaribu kuwaleta watu kwa Mungu, na kwenda mahospitalini na kuwazuru wagonjwa, na kujaribu kuwaleta watu kanisani na kutenda mema. Heri niwe na hilo kuliko mkusanyiko wa mengine yote; ijapokuwa hayo megine ni mazuri, ni mali ya kanisa."

170 Lakini kama ilinipasa niwe nalo, ningeweka hilo kwanza. Kwa sababu kama una hilo, mengine yatatendeka. Enhee. Ona? Kama una hilo, ukiwa na njaa sana kwa ajili ya Mungu, kupiga shangwe kutatukia. Ukiwa na njaa ya Mungu sana, kunena kwa lugha kutatukia. Ukiwa na njaa ya Mungu sana, utaendelea tu kuwa na njaa, uzidi kuwa nayo. Sasa, ukijiona haujali, kumbuka tu, jihadhari, kuna roho mwingine anayejaribu kutenda kazi ndani mle. Kaa mbele za Mungu, uwe mnyenyekevu, ukiwa na utungu wa nafsi. Uwe tu wa mtindo wa kale kweli kweli . . .

171 Naweza kuthibitisha kwa Biblia "Mara ya kwanza yule Malaika wa Bwana alipoenda kote nchini kutia alama kwa Roho Mtakatifu, Yeye aliwatia alama wale pekee waliolia na kuugua kwa ajili ya machukizo yaliyofanyika katika mji huo," Ezekieli, sura ya 9. Sivyo? Kutia hiyo alama katika vipaji vya nyuso zao wale wote wanaougua na kulia kwa ajili ya machukizo yanayofanyika katika mji huo.

172 Basi, nataka kuwaulizeni swali, nitawaulizeni swali hili. (Sasa tutafunga tu upesi niwezavyo.) Ingalikuwaje leo kama Roho Mtakatifu angalipita kote Jeffersonville, New Albany, na Louisville, kutia muhuri wale adhuhuri hii wangekuwa nyumbani, "Mungu, tuma mkutano wa ufufuo, tuna njaa sana kwa ajili ya mkutano. Ewe Mungu, tazama dhambi za mji huu. Ee, si zinachukiza sana, Mungu? Ee, nakusihi ukatutumie mkutano wa ufufuo, Mungu. Watume wahubiri wachache wazuri, tutumie mtu fulani. Ewe Bwana, na Roho Mtakatifu na . . . "? Wapi, Yeye angetia muhuri wapi? Waza hilo.

173 Sasa, "Vema, Ndugu Branham, wamaanisha nini?"

174 Nakusudia hili, nami nasema hili sasa kwa unyenyekevu, nikitembea kwenye nyuzi dhaifu. Naamini siku zimekaribia kwisha, wale walioko ndani wamo ndani. Ona? Ona? Milango yote inafungwa, huna mzigo huo tena.

175 Billy Graham alikuwa na mikutano nchini kote, na Oral Roberts, na wengine wetu sisi. Tumelia na kuomba na kuomba, na kadhalika. Lakini mwaona, milango inafungwa. "Mwenye uchafu," ninanukuu Maandiko, "azidi kuwa mchafu. Na mwenye haki na azidi kufanya haki. Na mtakatifu, azidi kutakaswa." Nami naamini milango ya Mataifa inafungwa. Ona? Siku za wakati wa majira hayo zimekaribia kwisha, ni wachache sana tu watakaoingia. Sababu huwezi kuwa na mkutano wa aina hiyo ni kwamba hamna utungu wa nafsi. Hu—hupati mzigo huo.

176 Nakumbuka miaka mingi iliyopita. Ninyi kila wakati huwasikia wakiongea kuhusu mikururo ya mavumbi ya mbao na kadhalika katika Maskani haya. Hiyo haikufaulu sana, sivyo hata kidogo. Lakini ilipokuwa jipya, Mungu alikuwa akiita Kanisa Lake. Nimewaona wao wakiugua na kulia na kulala madhabahuni usiku kucha. Nimeenda manyumbani mwao, na ungewasikia unapokuja, katika . . . katika vyumba vyao vya kulala, wanaume kwa wanawake, wakilia, "Ee Mungu!"

177 Ungewaona wao wakiingia kanisani, nami ningesikia kinanda kikiimba, *"Yesu unihifadhi,"* na machonzi yakitiririka chini pale, mwajua. [Ndugu Branham avuta hewa mapuani—Mh.] Naingia *humu* kanisani, kisha naenda kwenye kanisa lingine, na unawasikia wao kule, *"Hapo Msalabani,"* "Ee Mungu, mwokoe mwanangu okoa binti yangu, yeye amepotea, Bwana. Nakusihi!"

178 Hupati hayo tena. Kuna nini? Roho wa Mungu ameondolewa. Yesu alisema, alibashiri hili, kuwa upendo . . . kwa sababu upendo wa wengi . . . upendo wao utapoa. Kwamba kwa sababu ya kuongezeka maasi, upendo wa wengi utakwisha. Ona, ona, ungepoa, ungetoweka. Upendo unakufa. Na walichobakiza, ni taratibu tu; wanapiga kinanda juu chini, "Ee haleluya! Mungu atukuzwe! Haleluya! Na Bwana asifiwe!" Ona, hivyo tu, ni utaratibu tu. Usijidanganye mwenyewe, ona, ku—kujipumbaza mwenyewe. Ona, haidhuru hata tu . . . naenda hivi, ninaonge . . .

179 Sineni kuhusu Maskani yetu, nanena kuhusu yale ninayoona nchini Amerika. Imekuwa tu utaratibu, kuiga yale tuliyokuwa nayo. Na huo utungu wa nafsi karibu umeisha. Ee ndugu, dada, (Mungu, uturehemu) Mungu na aturehemu!

180 Tazama hii mikutano ya ufufuo na kadhalika ili—iliponda-ponda na kupondaponda na kupondaponda, na Injili ilihubiriwa dhahiri sana, ni . . . Itazame siku hizi, mara tu ufufuo ukwishapo, wanaondoka. Mwajua nini?

181 Hebu niseme hili. Sijui sababu gani siwezi kuondokea hili. Lakini, tazama, Yesu alisema, "Ufalme wa Mbinguni ni kama mtu aliyechukua juya na kulitupa majini. Naye alipolitupa, alichukua namna kadha ya baharini, bila shaka. Yeye alikusanya kasa, akakusanya nyoka, akakusanya kamba wa mtoni, na mbwa-maji, samaki. Ona? Nami naamini hilo juya . . .

182 Sasa, tazama! *Hapa* kuna kasa, *hapa* kuna samaki. Kasa huyo hawezi kujizuia kwa sababu yeye ni kasa, asili yake ni kasa. Tabia yake ni kasa, hakuna lingine. (Sasa kumbuka, ni-nilisema nitaomba.) Ona asili yake ni kasa, yeye ni kasa sasa. Kama asili yake ni nyoka, yeye ni nyoka sasa. Kama asili yake ni mbwa-maji . . .

183 Nami naamini kuwa juya limetupwa na kutupwa na kutupwa, hata karibu samaki wote wameondolewa kwenye kidimbwi.

184 Hiyo ndiyo sababu wao husema, "Vema, niliinua mikono yangu juu. Mungu atukuzwe! Nataka kuokoka. Bwana asifiwe!" Na siku kadha baadaye, "Ee, Lidia, wajua upuzi huo si... upumbavu...nalidhani ulikuwa sahihi." Mbona? Asili iliyoko *hapa* ni mbwa-maji, tangu mwanzo ni nyoka, asili yake.

185 Karibu samaki zimalizike baharini sasa. Juya litakaushwa. Na Yesu atakuja, ndipo Yeye atawachukua samaki Wake. Mwaona ninalokusudia? Ee, kama mna chembe moja ya Ukristo ndani yenu, kama mna hamu chembe moja kwako kumtumikia Mungu, ishikilie tu kwa dhati uwezavyo asubuhi hii na kuidhamini kwa moyo wako wote.

186 "Wana wa Mungu walijitwalia binti za wanadamu." Bila shaka wao walikuwa wana wa Mungu. Siku hizi wangali wana wa Mungu, bali wao ni wana wa Mungu walioanguka. Baadhi yao, kimaandiko, Whiu! Jinsi wawezavyo kunena Maandiko! Wao ni wana wa Mungu. Mwajua, Shetani alikuwa msaidizi mkubwa wa Mungu. Mwajua, yeye ajua Maandiko kuliko mwanatheologia ye yote—mwanatheologia ye yote ulimwenguni siku hizi. Waza...Yeye anazipindua seminari, hasa hii ya Batisti hapa inayosema kuwa—kuwa "Yesu Kristo alizaliwa na Mrumi, au askari Mjerumani." Nina kitabu kuhusu hayo, nataka niwaonyeshe hivi karibuni. Vema.

187 Upesi, Kutoka...Ee, hatungeweza kupata hilo ka—kamwe ijapokuwa turudi nyuma. Nitayajibu upesi sasa, najua nachukua wakati wenu mwingi. Mtanistamili kwa dakika chache zaidi? [Kusanyiko lasema, "Amina!"—Mh.]

13. Hao mia na arobaini na nne elfu, waliotajwa katika Ufunuo, ni wale masalio ya Wayahudi ambao tuta...watakuwa sehemu ya kule Kunyakuliwa kwa Kanisa? (upande wa pili) Si Israeli, mwanzoni mwa...walianza...(Nasikitika)... **wataingia katika wakati-wakati wa kule...**

188 Nasikitika, hebuni kidogo hata nitakapofaulu kusoma hili. Lilimepenyeza, limepenya karatasi.

> **...kutimia katika ile miaka elfu moja ya—ya Kristo kuliko ya kwamba mtu aweza kuishi kama hawa watu wa dini wa kisasa wafanyavyo,** Naam, bwana.

189 Sasa, hebu kidogo, nipate hili sahihi. Swali ni:

> **Je, wale mia na arobaini na nne elfu, ambao sisi ni masalio ya...**

190 Nataka tujisahihishe kwa hilo kwanza, hakikisheni ya kwamba mna...Ona, wale mia na arobaini na nne elfu...

> **Je, wale mia na arobaini na nne elfu, waliotajwa katika Ufunuo, ni wale masalio ya Wayahudi watakaokuwa sehemu ya kule Kunyakuliwa kwa Kanisa? Je, wale mia na arobaini na nne elfu...**

191 Sasa hebuni. . .Mimi—mimi nataka kushika hili dhahiri mawazoni mwangu kabla sijaanza kulijibu.

> **Je, wale mia na arobaini na nne elfu, waliotajwa katika Ufunuo, ni wale masalio ya Wayahudi wataokuwa sehemu ya kule Kunyakuliwa kwa Kanisa?**

192 Nataka kupata hayo kwanza. Wale mia na arobaini na nne elfu ni masalio ya Wayahudi, lakini si Kanisa litakalonyakuliwa. Ona? Tazama hapa sasa katika Ufunuo, sura ya 6, utaona hayo.

193 Ndipo tutapata sehemu nyingine upande mwingine—mwingine, nao wana swali lingine mle. Tazama mambo haya.

194 Vema, tazama hapa sasa, Ufunuo 6, sasa, hapo ndipo unapolipata. Ona? Sasa, tutaanza, yeye aenda mbele na kunena kuhusu wale wapanda farasi, na mengineyo, wakienda, "Walipofungua ule. . . " Hebu tupate kile kifungu cha 6 cha Ufunuo:

> *Na alipoifungua muhuri ya tano. . .*

195 Ni-nimekosea, niko katika sura nyingine. Ni sura ya 7:

> *. . .baada ya hayo nikaona malaika wanne wamesimama katika pembe nne za nchi.*

196 Ee, ni swali nzuri jinsi gani, na tuna wakati mchache jinsi gani kuliendea na kuwaombea wagonjwa.

> *. . .baada ya hayo nikaona malaika wanne wamesimama katika pembe nne za nchi, wakizizuia pepo nne za nchi, upepo usivume juu ya nchi, wala juu ya bahari, wala juu ya mti wo wote.*
>
> *Nikaona malaika mwingine, akipanda kutoka* mbinguni *mwenye muhuri wa Mungu aliye hai:. . .*

197 Ee, bila shaka, hili ni swali nzuri. Ona? Sasa, hiyo ni picha ya ajabu. Yohana alisema sasa, hapa. . . ametoka duniani sasa yumo katika Roho, akitazama nyuma duniani. Naye aliwaona malaika wanne wamesimama katika pembe nne za dunia, wakizizuia pepo nne za nchi.

198 Sasa, "pepo," katika Biblia. . .Sina wakati wa kuwasomeeni Maandiko. Lakini tunaweza kufikia hili. Kama halijajibiwa sahihi, ndipo nitalipata wakati mwingine. Zile nne. . .Pepo, katika Biblia, maana yake ni "vita na ugomvi." Kama katika wakati wa Ayubu, mwakumbuka, pepo zilishuka na—na kuwaua wale wana. Nanyi mwajua lile ninalomaanisha, ni—ni—ni matatizo. Ona?

> . . .na *nikaona malaika wanne (Malaika wanne,* au "wajumbe wanne.") *Walikuwa wamesimama katika* pembe za. . .au *pembe nne za nchi. . .wakizizuia pepo nne za nchi. . .*

> . . . *akawapigia kelele kwa sauti kuu wale malaika wanne waliopewa ku—kuidhuru nchi na bahari.* (Sasa huko ni kuja kwa Bwana, yale anayonena. Ona?)
>
> *Akisema, Msiidhuru nchi, wala bahari, wala miti, hata tutakapokwisha kuwatia muhuri watumwa wa Mungu wetu juu ya vipaji vya nyuso zao.* (watumwa).

199 Sasa, kumbuka, Kanisa si watumwa wake. Sisi tu wana wake, si watumwa Wake. Wayahudi kila mara ni watumwa Wake. Kanisa halijawahi kuwa watumwa Wake, limekuwa watoto Wake. Ona? Watumwa:

> *Nikasikia hesabu yao . . . waliotiwa muhuri katika kila kabila ya Waisraeli, watu mia na arobaini na nne elfu.* (sasa, tazama, wote ni Wayahudi).

200 Sasa tazama! "Wa kabila ya Yuda kumi na mbili elfu waliotiwa muhuri. Wakabila ya Reubeni, kumi na mbili. Wa kabila ya Gadi, kumi na mbili. Asheri kumi na mbili. Naftali kumi na mbili, na-na kuendelea. Simeoni, kumi na mbili. Na Asheri kumi na mbili. Na Zabuloni kumi na mbili. Na Benyamini, kumi na mbili." Na makabila kumi na mawili ya Israeli, kwa hivyo kumi na mbili mara kumi na mbili . . . ni ngapi? Mia na arobaini na nne elfu. Sasa, tazama, makabila yote ya wana wa Israeli. Sasa tazama, hao walikuwa "watumwa" wa Mungu.

201 Sasa labda naweza kufanya hili dhahiri. Sasa tazama:

> Baada ya hayo . . . tazama, *nikaona, na tazama, mkutano mkubwa sana ambao hapana mtu awezaye kuuhesabu,* (sasa, hapa kuna kundi lingine ona) *watu wa kila taifa . . . na kabila . . . na jamaa na lugha na watu, wamesimama mbele ya kile kiti cha enzi, na mbele za Mwana-Kondoo, wamevikwa mavazi meupe . . .* wana . . . *Mwana-Kondoo wamevikwa mavazi meupe, na wana matawi ya mitende mikononi mwao;*
>
> *Wakilia kwa sauti* kuu *wakisema, . . .* (Sikiza huu mkutano wa Roho Mtakatifu!) . . . *Wokovu una Mungu wetu aketiye katika kiti cha enzi, na Mwana-kondoo.*
>
> *Na malaika wote . . . wote walikuwa wakisimama pande zote—pande zote za kile kiti cha enzi, na za hao wazee, na za wale wenye uhai wanne, . . . nao wakaanguka kifulifuli mbele ya kile kiti cha enzi, wakamsujidu Mungu,*
>
> *Wakisema, Amina; Baraka, . . . utukufu . . . heshima . . . shukrani . . . heshima, . . . uweza, . . . nguvu, zina Mungu wetu hata milele na milele. Amina.*
>
> *Akajibu mmoja wa wale wazee . . .* (Sasa, tazama sasa, huyo alikuwa . . . Yohana alikuwa katika ono) . . . *mmoja wa wale wazee . . . akiniambia, Je! Ni akina nani . . .*

(Sasa, Yohana alikuwa Myahudi naye alipowaona wale makabila kumi na mawili ya Israeli aliwajua). . . Lakini *watu hawa waliovikwa mavazi meupe ni akina nani? nao wametoka wapi?* Wametoka wapi? Sasa umeona Wayahudi, wajua kila mmoja wao, uliwahesabu katika makabila na kueleza ni maelfu wangapi walitiwa muhuri. Lakini hawa ni nani wa kila taifa, lugha, na taifa? Wangetoka wapi?

Nikamwambia, Bwana, wajua wewe. (Yohana, kwa maneno mengine, "Sijui wanakotoka. Nami naona watu wangu—wangu na kuwaona hao walio hapa.") . . . *"Akaniambia, Hao ndio wanatoka katika dhiki ile iliyo kuu, . . . (Ona) . . . dhiki ile iliyo kuu, nao wamefua mavazi yao, na kuyafanya meupe katika damu* (si ufuasi wa makanisa) . . . bali *katika damu ya Mwana-Kondoo.* (Ona?)

Kwa hivyo wako mbele ya kiti cha enzi cha Mungu, nao wanamtumikia mchana na usiku katika hekalu: . . .

202 Sasa, Bi. Branham hunitumikia wapi? Nyumbani. Huyo ndiye Bibi-arusi. Bi. Neville, hapo ndipo akaapo, nyumbani, akikutumikia wewe. hapo ndipo Bibi-arusi (wao si watumwa) . . . Bibi-Arusi hutumika.

. . . katika hekalu, na yeye . . . aketiye katika kiti cha enzi atatanda hema yake juu yao.

Hawataona njaa tena, . . . (walikosa milo michache, inaonekana (sivyo?) walipokuwa hapa) . . . *njaa tena, wala hawataona kiu tena, . . . wala jua halitawapiga, wala hari iliyo yote.*

Kwa maana huyo Mwana-Kondoo, aliye katikati yao atawachunga, naye atawaongoza kwenye— *yenye uhai* . . . (hebu kidogo) . . . *chemchemi za maji yenye uhai, na Mungu atayafuta . . . machozi yote* (hilo lililoingia mle ni kundi linalolia) *katika macho yao.* (Ona?)

203 Sasa, tazama, walikuwa na njaa na kiu, na vilo, na maombolezo na kuomba-omba, walitoka kwenye dhiki (kasema, "Tazama hilo kundi la watakatifu wanaojigaragaza, ee, wana kichaa!) Jamani! Naam. Ona? Lakini walilia na kuomba-omba, hawakugombana wala kuzozana. Nao walilia tu na kuomba-omba. Basi, ona, nao walikuwa wa jamaa yote na lugha, na taifa.

204 Sasa, wale mia na arobaini na nne elfu, hao walikuwa Wayahudi. Ibrahimu alikuwa mtumwa wa Mungu. Wayahudi kila mara wamekuwa watumwa wa Mungu. Mataifa hawajawahi kuwa watumwa Wake.

205 Sasa, yanipasa niharakishe kumaliza hili sasa, kwa sababu tunayo mawili matatu zaidi. Nami nitaharakisha upesi

niwezavyo, na si kujaribu kuyaruka haya. Lakini nitarudi na kuyajibu tena Jumapili ijayo (Bwana akipenda) na kuchukua wakati mwingi kwayo.

206 Lakini, tazama sasa, yeye aliona pembe nne za nchi, na hao malaika wamesimama katika pembe nne za nchi. Sasa, unasema, “Nilidhani ilikuwa mviringo,” hiyo si kusema haina pembe nne, mwaona. Vema.

207 Sasa, “Kwenye pembe nne za nchi, wakizizuia zile pepo nne.” Kwa maneno mengine, pepo zilivuma, zikivumisha vita na misukosuko iliyokuja ulimwenguni kote. Hayo yalitimia lini? Hayakutimia hata vile Vita vya Kwanza vya Dunia. “Kuzuia pepo,” nao walikuwa wakijitahidi, kuitwaa.

208 Na sasa, hapa yuaja mwingine mmoja. Sasa, ukitazama na kumkumbuka huyo Malaika, ni Malaika yule yule aliyejitokeza katika Ezekieli 9, watu walipokuja toka nyuma ya malango yao wakiwa na vitu vyao vya kufisha waliopita Yerusalemu kote kuwaangamiza Wayahudi. Mwakumbuka? Yeye alisema, “Zuia! Zuia! Komesha, hata utakapoenda mjini kote na kutia alama kwa kila paji la uso linalougua na kulia kwa ajili ya machukizo yafanywayo katika mji huu.” Sivyo?

209 Basi, Yeye alipokwisha kufanya hayo, ndipo aliwaruhusu waingie na kuangamiza. Hayo yalikuwa yale mateso yaliyoongozwa na Tito. Sasa, mwaona, yeye ni Malaika yule yule, aliyejitokeza tena, akitoka Mashariki (na ndiko Yesu atakakotokea) mwenye Muhuri wa Mungu Aishiye. Utukufu!

210 Sasa, Muhuri wa Mungu Aliye hai ni nini? Ee, kama huo si mzozo mkuu ulimwenguni siku hizi! Wengine husema ni kuadhimisha siku ya sabato, na wengine husema ni kufanya *hili* na *lile*. Lakini Biblia ilisema, “Roho Mtakatifu ndiye Muhuri wa Mungu”! Waefeso 4:30 yasema, “Msimhuzunishe yule Roho Mtakatifu ambaye mmetiwa muhuri hadi ile siku ya ukombozi wenu.” Ona? Vema. Ni Roho Mtakatifu.

211 Ndipo ikawa vipi? Sasa, tazama! Ee, niwazapo hili, moyo wangu huruka. Sasa, Yeye alisema, “Zuia zile pepo nne hata,” (kwa maneno mengine) “tutakapowatia muhuri watumishi wa Mungu wetu kwenye vipaji vya nyuso zao.” *Watumwa,* ni “Wayahudi.” (Yohana akageuka kasema, “Naliona wale mia na arobaini na nne elfu wametiwa muhuri.”) Sasa, zile pepo zote zikavuma, na zingefunika nchi yote na vile vita vya Amagedoni vingetokea katika vile Vita vya Kwanza Dunia, lakini . . .

212 Sasa yanipasa kuchukua Andiko jingine hapa kuwaonyesheni ninyi. Yesu alinena kuhusu watu ambao . . . Yeye alisema, “Wengine wataingia kwa saa moja, na wengine kwa saa nyingine, nao walikuwa watu wa saa ya kumi na moja. Watu wa saa ya kumi na moja.” Sasa, ninyi mlio wa kiroho someni katikati ya mistari, kwa sababu yanipasa niruke hapa na kuharakisha. Sasa, tazama. “Wakaingia, hao watu wa saa

ya kumi na moja." Na sasa hivi. . . "Wa kwanza wakaingia na kupata senti, na wa pili wakaingia nao wakapokea senti, nao watu wa saa kumi na moja wakapokea senti ile ile kama hao walioingia kwanza." Sivyo? Ile saa ya kumi na moja!

213 Sasa, tazama, Wayahudi ndio jiwe la kuonyesha maili njiani tunalofuata sasa. Naam, Vita vya Kwanza vya Dunia vilipotokea, vilichukua kila Myahudi, walitawanyika katika mataifa yote. Kama Andiko la kwanza lililoulizwa leo, jinsi Yeye angewatawanya katika mataifa yote, wote wamo mle. Na hapa kukaja pepo zile zikiingia Yerusalemu, kila mahali, vita vya dunia.

214 Naye alisema, "Zuia! Vikomeshe, hata tutakapokwisha kuwatia muhuri hao watumwa wa Mungu wetu." Kwa maneno mengine, "Tunawaleta humu toka mataifa yote, kila mahali, kuwaleta humu kwa sababu yatupasa kuwaingiza moja kwa moja ndani humu kutia muhuri wale mia na arobaini na nne elfu. Zizuieni."

215 Na Vita hivyo vya Kwanza vya Dunia vikakomeshwa mwezi wa kumi na moja wa mwaka, siku ya kumi na moja ya mwezi, saa kumi na moja, kusudi watu wa saa kumi na moja wapate kuingia. Wito wa mwisho kwa Myahudi! Naye atapokea ubatizo ule ule wa Roho Mtakatifu walioupata mwanzoni nyuma kule siku ya Pentekoste, wabatizwe vivyo hivyo, na kadhalika, watu wa saa kumi na moja wanaingia.

216 Yeye alisema, "Zuia, sasa, hata tutakapotia muhuri."

"Utazizuia kwa muda gani?"

217 "Hata tutakapokwisha kuwatia muhuri watumwa wa Mungu wetu. Sasa, sisi—tunatia muhuri Mataifa, wamekwisha kutiwa muhuri, maelfu mara elfu kupitia kwa mateso na dhiki, wametiwa muhuri. Lakini ngoja kidogo! Kitambo kidogo! Usiache mat. . . Wakati usiishe hata tutakapokwisha kuwatia muhuri hao watumwa." Naye akatia muhuri wale mia na arobaini na nne elfu.

218 Ndipo pepo zile zikaachiliwa tena. Sasa, tazama, na tangu vile Vita Vya Kwanza Vya Dunia daima kumekuwa na mateso dhidi ya Wayahudi. Kukazuka Hitler kwa ajili ya vile Vita Vya Pili Vya Dunia, naye alipoinuka, alianza ku. . . Nini? Yeye angaliiangamiza dunia nzima. Sivyo? Angaliiangamiza, yote. Naam, angaliiangamiza.

219 Kila kitu ilibidi kiwe Ukomunisti. Je, mwakumbuka mlipokuwa mkitaka kunitupa korokoroni chini hapa? Nilikuwa ni—nikihubiri jambo hili hili chini hapa kwenye kilinge cha mtoni usiku huo. Naam, bwana. Nikisema, "Kutakuwako na aina tatu za kisiasa. Na zote zingerundikana pamoja katika moja, na muungano huo ungeleta mateso ambayo yangemrudisha tena Yesu Kristo duniani." Na hiyo ni kweli hasa. Na huo ulikuwa Ukomunisti, na—na Hitler na—na Nazi, na kadhalika; na jinsi

huo Ufashisti wa Mussolini, na Hitler, na Stalin. Nilisema, "Moja ya hayo litatimia. Sijui itakuwa lipi, lakini naamini itakuwa yule mfalme wa Kaskazini." Hakika mwakumbuka mambo hayo na jinsi hayo yamefundishwa ndani humu; na ndugu Mahoney, nanyi nyote mlio kule nyuma kabisa.

220 Nao wakasema, "Ukihubiri hayo . . . "

221 Na kwa hili jambo la N.R.A., nilisema, "Hiyo si chapa ya mnyama, siyo kamwe. Ni mgomo wa kidini; si hilo." Nilisema, "Hiyo ni tangulizi ya kuwatayarisha watu, na kujua kuwa ni mwanzo tu. Papa hapa ndipo mwanzoni mwa huzuni, papa hapa ndipo tunapoanzia. Papa hapa ndipo wakati—wakati uanzapo kuwadia. Sasa, tazama, hapo wakati huo."

222 Basi mateso yakawajilia Wayahudi nao wakaanza kuwatesa wao toka kila taifa na kuwasukumiza katika Yerusalemu. Sivyo? Kila mmoja, wanaendelea moja kwa moja . . . Na utakuwa na mia na arobaini na nne elfu. Tazama hapa kidogo katika Ufunuo ambapo Yohana . . .

223 Bw. Bohanon chini hapa aliniambia, kasema, "Singesoma kitabu cha Ufunuo." Kasema, "Huku Bibi arusi amesimama kwenye ule Mlima Sinai." Kasema, "Huku Bibi-arusi yumo Mbinguni." Na kasema, "Ndiye huyo Bibi-arusi na yale maji . . . yule joka mkubwa akitoa maji toka kinywani mwake kufanya kufanya vita naye." Akasema . . .

224 Nikasema, "Bw. Bohanon, jambo la kwanza ni kwamba, umepata kitu kisicho sahihi, ukakiita "Bibi-arusi.' Nilisema, "Hao Wayahudi watasimama kwenye Mlima Sinai, hao mia na arobaini na nne elfu. Bibi-arusi, bila shaka, alikuwa Mbinguni pamoja na Yesu. Na yule joka aliyetoa maji toka kinywani mwake atafanya vita na *masalio* ya mzao wa mwanamke." Hilo lilikuwa *hili* kundi hapa lililopaswa kurudi chini, si *hilo*. Ona? *masalio* ya Uzao wa mwanamke, "kanisa lililotakaswa," pasipo kupokea Roho Mtakatifu, hao ndio aliofanya vita nao. Ona?

225 Ndio hawa, ndio hawa hao makabila matatu. Usisahau matatu daima. Na *hapa* twaona, kote, hawa mia na arobaini na nne elfu, wakimzunguka huyo Bibi-arusi mkuu aliyekombolewa. Ndio hawa masalio waliyoachwa, ndio hao, wao ni Wayahudi, bado kungali kuna wale mia na arobaini na nne elfu. Hawa ndio wale waliotakaswa, waliokataa kumpokea Roho Mtakatifu. Kanisa litawatesa . . . Ka—kanisa la Kirumi na wengineo watawatesa hao, lakini Bibi-arusi amekwisha kunyakuliwa na yumo Mbinguni. Ndio hao, wamewekwa jinsi Biblia ilisema wangekuwa. Ona?

226 Kwa hivyo wale mia na arobaini na nne elfu ni Wayahudi, watumwa wa Mungu. Na watakapohubiriwa Injili ya Roho Mtakatifu nao wapokee ubatizo wa Roho Mtakatifu jinsi hasa walivyofanya mwanzoni, majira ya Mataifa yametimia, Kanisa limetiwa muhuri, kule Kunyakuliwa kwaja.

227 Siku za Mataifa, Injili imehubiriwa kila mahali, imehubiriwa kwa nguvu katika Mataifa, kuvuta huo wavu mkubwa, kujaribu kupata kila samaki aliyeko majini aingie. Na watazame, wakubwa sana. . .?. . .Mvuo wote ulikuwa kasa na kenge wa majini, na kadhalika. Mara tu mkutano wa ufufuo ukwishapo wanarudi moja kwa moja tena katika ulimwengu. Karibu samaki zimekwisha. Mwaona lile ninalomaanisha?

228 Injili imekwisha kuhubiriwa! Husikii kulia tena, hakuna tena maombolezo, hakuna tena kuugua, kulia kwa ajili ya ubatizo wa Roho Mtakatifu. Wanapenda kuingia, nawawekee mikono yao midogo kwa mamia, nao wanafanya yasiyofaa kuchezacheza, labda, au kitu kama hicho. Ni sawa, lakini hayo ni matokeo yake tu.

229 Utu wa Kristo Yesu huzaa kitu halisi, na kumweka mtu huyo salama katika Kristo hata atakapokuja. Ndiye Huyo. Na sasa, hiyo ndiyo sababu hakuna kulia tena, milango karibu imefungwa. Ujumbe umesambazwa, ni karibu wakati wake wa mwisho, mivuto michache tu hivyo kuwaingiza katika Ufalme wa Mungu. Milango inafungwa!

230 Ndipo jambo linafuata? Wayahudi wapaswa kumpokea Roho Mtakatifu na wabatizwe kwa Jina Lake Yesu Kristo. Kote kote wameteswa na kudhihakiwa; na, pale, mara tu Roho Mtakatifu atakapohubiriwa kwao, watapokea ubatizo wa Roho Mtakatifu. Kanisa la Mataifa limekwisha kunyakuliwa. Na wale waliokataa, na kuenenda tu chini ya kuhesabiwa haki, yule joka (zile nguvu za Kirumi) anatema maji, ambayo yataunganika na Ukomunisti, na kuliingiza kanisa katika mateso hivyo. Ndiyo hiyo picha yao hasa.

231 Ee ndugu, tunapoiona ikija, hiyo ndiyo sababu ninaomba, hiyo ndiyo sababu namlilia Mungu, "Bwana, hebu niwaendee Wayahudi hao. Hebu nianzie kule Afrika, nifanye kazi kwa majuma machache kwa hao Mataifa na Waislamu. Na niende kule India na nijaribu kuonyesha na kuwadhihirishia wao Bwana Yesu Kristo halisi kwa nguvu Zake, miujiza Yake, ubatizo Wake, kila kitu, na Roho Mtakatifu." Ndipo tutakapofika Yerusalemu. . .

232 Ndugu Beeler, hili ndilo ulilokuwa ukiuliza. Watakapokuja Yerusalemu na kusimama nje pale, na kusema, "Basi, kama Yesu ni Mwana wa Mungu aliyefufuka toka kwa wafu, Yeye anajua mambo kama alivyofanya nyuma kule mwanzoni, Yeye aweza kutoa Uzima ule ule ambao aliuotoa nyuma kule. Na kama akifanya hivyo, mtamkubali Yeye kama Mwokozi wenu binafsi?" Na ndipo ionyeshwe ya kwamba Mungu kwa nguvu kuu na vinginevyo vya nguvu za kufufuka Kwake, Yeye yu pamoja nasi.

233 Ndipo wafanyapo hayo, niseme, "Jamani, ninyi mliompokea Yeye kama Mwokozi wenu binafsi. . ." Natumai kutakuwa na

maelfu yao. Niseme, "Roho Mtakatifu yule yule aliyeshuka kwenye siku ya Pentekoste yu papa hapa kwa ajili yenu."

234 Ndipo Injili itawarudia Wayahudi papo hapo wakati huo. Kisha kutakuwako ufufuo kati ya Wayahudi hao papo hapo ambao utabeba maelfu na makumi elfu na . . . mia na arobaini na nne elfu, katika ule Ufalme wa Mungu, watatiwa muhuri na yule Malaika mwenye kutia muhuri.

235 Natumai kuwa Yeye yuaja toka Mashariki. Hivyo ndivyo Yeye alivyo kwetu sasa, ameshika muhuri Wake mkononi Mwake. Ndipo, lo, nataka nikusanywe mle. "Nimetuma mateso hapa na mateso pale, nami nimewafukuza Wayahudi na kuwafukuza kwa nguvu niwezavyo. Nao wemerudi mle. Wayahudi wengi nchini Amerika (ambao hawataweza kutoroka) wamekwisha kupokea Roho Mtakatifu. Lakini nina wale wote mia na arobaini na nne elfu mle watakaopokea ubatizo wa Roho Mtakatifu."

236 Na papo, mara tu yule Malaika mwenye kutia muhuri—atakapoanza kutia muhuri hao mia na arobaini na nne elfu, mlango wa Kanisa la Mataifa umeshafungwa, nao Wayahudi wanawapelekea Wayahudi wengine Roho Mtakatifu. Nao watakuwa na mkutano wa ufufuo utakaoenea duniani kote. Haleluya! Na nguvu za Mungu zitadhihirishwa miongoni mwa Wayahudi. Ee, ajabu vipi! Whiu! Jamani!

237 Hebu nione, hiyo inatuelekeza kwa Isaya. Nasi tulipata hilo "wana wa Mungu." Sasa hebu tuone.

Si Israeli . . .

238 Ona kama unaweza kusoma hilo, ndugu. Mimi . . . laonekana limeandikwa-andikwa, yeye alifuta mara kadha. Huku nami nikitafuta lingine. Ukiweza, tafadhali [Ndugu Neville asoma swali linalofuata—Mh.]

14. Si Isaya anamaanisha kwa "kuisha kwa upanga," anakusudia ufanisi utakaokuwemo katika ule Utawala wa Kristo miaka elfu, sio kitu ambacho mwanadamu angefanikisha (kama vile dini nyingi sana za kisasa hutwambia)?

239 Ye yote uliye, ndugu yangu mpendwa au dada . . . waonekana kama mwandiko wa mwanamume. Lakini, haidhuru, ye yote uliye, umesema kweli hasa! Hapo ndipo majembe yatakapofuliwa . . . au panga zitakapofuliwa ziwe majembe. Hiyo itauleta ule Utawala wa Miaka Elfu. Na dini zote za kisasa zilizojitenga zinazozunguka hapa na pale kujaribu kuwaelimisha watu wakaingie Ufalme wa Mungu . . . Hiyo itakuwa wakati Mungu Mwenyewe atakapokuja katika Mwili wa kimbinguni na katika Nguvu za kimbinguni zitakazowafinyanga wana wa Mungu. Haleluya! Hakutakuwako tena na kusoma, kuandika, hesabu, itakuwa kwa nguvu za kufufuka Kwake Yesu Kristo. Ndipo ulimwengu hautajifunza tena vita kamwe.

240 Kila taifa siku hizi, kila tawala, kila ufalme vinaongozwa na lbilisi. Biblia ilisema hivyo. Na hivi karibuni ufalme wa ulimwengu huu utakuwa falme za Bwana wetu na Kristo Wake, naye ataongoza na kutawala miaka elfu moja duniani; na kulinyakua Kanisa. Bila shaka, hiyo ni kweli hasa, msomaji mpendwa.

241 Wale mia na arobaini na nne elfu ni watumwa. Hesabu kubwa ambayo hakuna mtu awe . . . "Makutano ambayo hapana mtu awezaye kuyahesabu," ni Mataifa.

242 Hebu kidogo sasa, jambo moja zaidi pale. Siwezi. Nitakuwa tu na maombi ya kusanyiko lote basi, katika muda mchache. Tazama hapa, nafikiri hili ni muhimu zaidi hivi sasa. Nataka kuwaombea wangojwa, lakini tutaharakisha. Badala ya kuwa na upambanuzi, tutawaombea tu. Nataka kuwaulizeni jambo fulani. Je, kuna lingine pia? Nitachukua hili tu na kuendelea Jumapili ijayo, nadhani.

243 Tazama, marafiki, kuhusu hili, ni nzuri jinsi gani! Tazama! Nawatakeni ninyi mtazame sasa, kwa makini, mtu huyu aliyeuliza swali hili. Wale mia na arobaini na nne elfu, sasa, hao ni watumwa, watatumika. Ungalichunguza, mahali pake, katika Maandiko ya kale . . .

244 Kila mara Tazama vivuli ukitaka kuona kitu chenyewe halisi kilivyo. Naam. Tazama nyuma kule, ona ni nini. Sasa, hilo ni kadhalika tangu Msalaba, na tazama chenyewe halisi kilivyo ukitaka kuona kivuli ni nini. Nyuma kule, ilikuwa ni kuegemea Msalabani, ilitupasa kutazama (nyuma kule) kuona hicho kivuli, kuona msalaba ungekuwaje; sasa yakupasa utazame toka Msalabani, kutazama nyuma na kuona jinsi kivuli kilivyo. Ona? Tazama jinsi Kristo alivyokuwa katika siku zile Yeye alipokuwa hapa duniani, Yeye alivyokuwa wakati huo ndivyo alivyo sasa. Hiki ni kivuli Chake. Mwaona lile ninalomaanisha? Mwajua, mwanzoni nilipolieleza, hivyo ndivyo lilivyo. Sasa, kama ninatazama toka nyuma kule, yanipasa kutazama jinsi kivuli kilivyokuwa kutambua hili litakuwa nini, jinsi Msalaba ulivyokuwa.

245 Sasa, siku moja kulikuwako na dhambi katika Israeli, na kulikuwako na mtu . . . wa kabila liitwalo Lawi. Walichomoa panga zao wakaenda na Musa kambini, nao wakaharibu kila kitu kilichokuwa dhambi. Sivyo? Mungu akatazama chini na kusema, "Kwa sababu mlifanya hili na kunitetea Mimi yako . . . hawa wengine wote watawatumikia ninyi. Nanyi ingieni katika hekalu kama makuhani." Sivyo? "Mkae papo hapo hekaluni, na wengine wao watafanya kazi na wataleta sehemu ya kumi na kuwatumikieni ninyi." Sivyo?

246 Ee, haleluya! Kama unaweza kuona vile hilo hekalu lilivyokuwa, ambamo hao Walawi walikuwa Bibi-arusi. Sasa, dhambi inapoinuka toka kila upande, Walawi wanachomoa

panga zao. Bibi-arusi aliyezaliwa na Roho Mtakatifu amesimama wima, akisema, "Yesu Kristo katika iliyo halisi ni Yesu Kristo katika ya kivuli, ni Yeye yule tu. Dhambi bado ni dhambi, ni kosa kufanya mambo haya!" Naam, wanasimama pale wameshika Upanga.

247 Mungu asema, "Njooni sasa, mlio wabarikiwa wa Baba yenu." Huyo ni Bibi-arusi.

248 Ndio hao watumwa, kisha tazama ambapo watumwa walipiga kambi. Kumi na mbili upande huu . . . Namaanisha, wanne upande *huu*, wanne upande *ule,* wanne upande *huo* na wanne upande *huo*; makabila kumi na mawili. Makabila kumi na mawili ni wale mia na arobaini na nne elfu. Tazama katika Kitabu cha Ufunuo, yeye aliona Mji ule ukiwa na misingi yake kumi na miwili. Juu ya kila lango mlikuwa na jina la mtume, na malango kumi na mawili. Na kando yake kulikuwa na yale makabila kumi na mawili, (haleluya!), yameyazunguka.

249 Na ndani mle kulikuwa wale Waliokombolewa. Haleluya! Weusi, weupe, manjano, kahawia, na wote waliooshwa kwa Damu watakuwa watumwa Wake, Yeye alisema watakuwa pamoja Naye. Wata . . . jua halitawaangazia tena, hawatasikia njaa wala kuona kiu tena, na katika Wakati huo mkuu na usio na mwisho wao wataishi na kutawala pamoja na Kristo milele; Yeye, aliye Mfalme; nao, walio Malkia. Wataongoza na kutawala milele!

250 Bwana awabariki. Amina. Nitaweka haya; Mungu akipenda, nitayajibu tena, labda usiku huu, na kuyajibu usiku huu au wo wote Ndugu . . . tutakusanyika pamoja na kuzungumziana. Bwana awabariki. Mwampenda Yeye kwa moyo wenu wote?

Ee, nataka kumwone, kuutazama uso Wake,
Huko niishi milele kwa neema Yake ya iokoayo;
Kwenye njia za utukufuni nikapaze sauti yangu;
Masumbuko yote yamekwisha, hatimaye nimo nyumbani, raha daima (Ee, lo!)
Nisafiripo duniani hapa, nikiimba ninapoenda,
Nikielekeza watu Kalvari, kwenye kile kijito chekundu, (si—si kanisani; kalvari)

251 Huko ndiko tunakowaelekeza; si kwa theologia fulani, lakini kwa hicho kijito chekundu, kwa Yesu Kristo. "Uhai u katika hiyo damu," na Yeye ni Damu ya Mungu ambayo ndiyo Uhai wetu unaoishi ndani yetu sasa. Kibarikiwe kifungo kitufungiacho!

252 Hali tukienda kuombea wagonjwa, nataka wimbo ma—maalum sasa hivi. Nataka Dada Gertie na binti yake, wakiweza, waje hapa. Na huu ni wimbo wa asili wa kale, nawatakeni mniimbie, *Amini tu*. Nakumbuka, nilikuwa nikiingia pale mlangoni, na wimbo huu umenifuata kote duniani. Nami—nami

nawataka wauimbe, yeye alikuwa wa kwanza kuuimba, mara ya kwanza nilipousikia. Rafiki msiri wangu alivandika, Paul Rader. Na, kabla hatujawaombea wagonjwa, nawataka wao wauimbe huku baraka Zake Mungu zikitulia juu ya watu walio wagonjwa.

253 Tumechukua wakati mwingi sana. Samahani, Ndugu Neville. Mungu awabariki. Mnapenda maswali? Nayapenda. Ee, na hayo yalikuwa mazuri sana, yalikuwa mazuri kabisa. Na mna kundi lingine. Na bila shaka, mengine yao hayajajibiwa vilivyo bado, lo, tungesema mengi sana juu yake. Lakini Bwana na awabariki.

254 Ninyi nyote wekeni nia zenu kwa Yesu Kristo sasa, na hebu tuache maswali tugeukie uponyaji wa Kiungu. Wangapi walioko hapa wanataka kuombewa? Hebu tuone mikono yenu, wanaotaka kuombewa. Vema, tutawaleta mbele na kuwaombea kwa muda mchache, mara tu, dada zetu waimbapo huu wimbo mtamu. Wanapojitayarisha, kinachoning'inia papo hapo juu yenu sasa ni ile Ahadi, hii ni Biblia Yake. [Dada Gertie na binti yake waimba *Amini Tu*—Mh.]

Amini tu, ami . . .

255 Sasa, ninyi mlio wagonjwa, songeni huku juu kuzunguka madhabahuni sasa, mkiweza.

Yote yatendeka, amini tu;
Amini tu, amini tu,
Yote yatendeka, amini tu,

256 [Ndugu Branham aanza kuuvumisha *Amini Tu*—Mh.] Sasa, Baba wa Mbinguni, tuna shukrani sana leo kwa ajili ya Maandiko haya na kwa ajili ya wimbo huu, "Amini tu." Tunaweza kukusikia wewe ukimwambia yule baba aliyekuwa na mwana mwenye ugonjwa wa kifafa, "Amini tu, yote yatendeka."

257 Sasa, twaomba, Mungu, watu hawa wanapokuja kuombewa, kwamba tuko hapa, kivuli, kivuli tu; ile iliyo halisi imetuzunguka sisi, yule Roho aishiye milele aliyekuwa juu yetu hatakufa kamwe. Itakuwa ni yote katika nyakati zote bila kikomo. Nasi twasonga mbele sasa kama mtumishi wako aliyetiwa mafuta, kusaidia watu wenzi wetu wapate msaada, kwa jambo moja pekee, Baba, ya kwamba watakutukuza wewe. Na sasa na kila mmoja anayesimama hapa madhabahuni asubuhi hii, mgonjwa, anayeugua, sasa na Roho Mtakatifu atoe uponyaji kwa kila mmoja wao.

258 Na sisi kama kundi Lako ndogo—ndogo, ambalo dada hawa walikuwa wakiimba wimbo wake, "Msiogope, enyi kundi ndogo," twajua, Bwana, umeona vema kuwapa hao ule Ufalme. Nasi twajua kuwa Wewe kila mara u karibu, kwa kuwa Wewe ulisema, "Walipo wawili watatu wamekusanyika kwa Jina Langu, nami nipo papo hapo katikati yao. Na lo lote waombalo, nitawapa."

259 Sasa, kulingana na Neno la Mungu ambalo haliwezi kutanguka, Neno la Mungu, mjalie kila mmoja uponyaji, Bwana. Nao wamesimama hapa, wakingojea. Tunapoenda kuwapaka mafuta na kuwawekea mikono, na kuomba ukombozi, na kila mmoja wao aende kitini mwake, warudi manyumbani mwao, wakikusifu Wewe, (wamepata nafuu, wamepona, na wazima), na warudi tena usiku huu, Bwana, mkutanoni, watoe sifa na utukufu kwa Mungu kwa ajili ya uponyaji wao. Tujalie, Bwana.

Na tunapoinamisha vichwa vyetu:

260 Ndugu Neville, njoo pamoja nami, ukiweza. Nataka Ndugu Fleeman, na Ndugu . . . shemasi, au mtu fulani hapa, na Ndugu Cox, ninyi nyote njooni hapa mkanisaidie. Ni mashemasi wote hapa wa kanisa hili ninaowaita wakati huu.

261 Na tunapowaombea, mnaweza kuwasaidia mkitaka. Ni—ninataka kila mmoja ndani humu awe mnyofu sana. Na tunapowaombea, mnaweza kuwasaidia mkitaka. Ni—ninataka kila mmoja ndani humu awe mnyofu sana. Na tunapowaombea wagonjwa, nawatakeni mwombe pamoja nasi.

262 Namwona mvulana mdogo anayeketi nyuma pale sasa, ambaye mudam chache uliopita aliingia kwenye jumba hili pale naye alikuwa na kutokwa na damu. Na Bwana Yesu ameikomesha hiyo damu kabisa sasa hivi. Ona? Rehema Zake zisifiwe, Jina Lake liheshimiwe. Angalieni ni wangapi wamepona katika siku chache zilizopita.

263 Waza tu Bwana Yesu yule yule aliyekuwa nyuma kule katika siku za mitume yuko papa hapa sasa. Na mwisho wa Mataifa unamalizika. Kazi kuu inaendelea miongoni mwa wanaoamini ya kimbinguni, sababu twaamini kuwa Mungu yuko hapa.

264 Waza tu, mwili wako—wako uliotukuzwa uko papa hapa Maskanini sasa, ule Uwepo wa Roho Mtakatifu ambao ndio hali yako iliyotukuzwa. Umetukuzwa katika Kristo sasa hivi! "Wale Yeye aliowahesabia haki, hao akawatukuza." Na mwili wako uliotukuzwa unasimama karibu nawe sasa hivi, katika Kristo Yesu, kukupa wewe nguvu kama ya umeme ukiingizwa katika chombo chake. Roho Mtakatifu yumo ndani yako. Ni umeme mwilini mwako kukupa wewe nguvu mpya, kukuponya kwa magonjwa uliyo nayo, kukupa nafuu.

265 Sasa, nataka kanisa, kama wataweza, na dada zetu, kama watauimba wimbo huu wote tena. Naam, kila mmoja wenu madhabahuni . . .

266 Sasa, marafiki, kama mimi ni mdanganyifu, mimi sina habari. Ninajaribu kuwa Mkristo, na kwa moyo wangu wote ninajaribu kuwasaidia watu. Nami najaribu kuwasaidieni ninyi. Watoto wa Mungu. Na kama mimi—kama mimi nampenda Baba yangu wa Mbinguni, nitawapenda ninyi, watoto Wake, kama Si . . . Kama ninawadanganya ninyi, nimejaribu kumdanganya

Mungu, ninyi ni watoto Wake; hakuna ye yote awezaye kumdanganya Mungu. Najaribu kuwasaidieni.

267 Hiyo ndiyo sababu Mungu anabariki juhudi zangu. Na labda zingine ni hafifu sana, na baadhi yazo zinaniaibisha, na Mungu ajua nazionea aibu na kutubu kwa ajili ya juhudi zangu. Lakini nafanya yote niwezayo kuusaidia Ufalme wa Mungu na kuwasaidieni ninyi watoto Wake. Mpokeeni Yesu asubuhi hii kama Mponya wenu, papa hapa jukwaani, mtarudi vitini mwenu na nyumbani kwenu mkiwa wazima na mkapate nafuu.

268 Sasa, kama Yeye ataponya mamia hapa, na maelfu na maelfu kote ulimwenguni, mbona Yeye asikuponye wewe? Amini tu. Vema, kina dada. Ndugu Neville, nakutaka wewe uje na uwapake hawa mafuta. [Ndugu Branham na ndugu wengine waombea wagonjwa. Dada Gertie na binti yake waimba *"Amini Tu"*—Mh.] . . .? . . .

Mwenendo, Utaratibu Mafundisho ya Kanisa, Kitabu Cha Kwanza
(Conduct, Order And Doctrine Of The Church, Volume One)

Jumbe hiza za Ndugu William Marrion Branham, ziliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali zilitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings. Ilichapishwa tena katika mwaka wa 2013.

SWAHILI

©2009 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings

P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.

www.branham.org